WAKATI WA FURAHA

SIKU YA KUKUMBUKA

YALIYOMO

Mwanzo wa Furaha……. 1

Mzunguko wa Wiki……. 6

Tangu mwanzo wa wakati…….. 10

Siku ya kukumbuka…… 12

Naye akaja Nazareti…… 19

Kutoka huzuni hadi furaha……. 23

Mawingu kwenye mstari wa upeo wa macho…… 32

Katika mazingira…… 38

Furaha milele……. 44

Siku ya kupendeza……. 47

Maungamo Dhahiri…… 61

Biblia inasema…… 72

Maswali ya kutafakari yajibiwa……. 82

Siku ya furaha……. 86

MWANZO WA FURAHA

"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi."

Dunia ilipotoka mikononi mwa muumba wake, ilikuwa inapendeza sana. Uso wake ulitofautishwa kwa milima, miinuko na tambarare, vikitenganishwa na mito mizuri na maziwa yenye kupendeza; lakini vilima na milima haikuwa yenye kutokeza ghafla na isiyolinganan, yenye miinuko mikubwa na nyufa au mapango ya kutisha, kama navyoonekana sasa; ncha kali, zisizolingana za miundo ya miamba ya dunia zilifunikwa chini ya ardhi yenye rutuba, ambayo kila mahali ilitoa ukuaji wa kupendeza wa mimea ya kijani. Jeshi la malaika liliangalia onyesho hili kwa furaha, na walifurahia kazi ya Mungu ya ajabu.

Baada ya dunia na wingi wake wa viumbe hai vya wanyama na mimea vilipokwisha kuweo, mtu, ambaye ni kilele cha kazi ya Muumbaji, na ambaye kwa jili yake dunia nzuri ilikuwa imeandaliwa, aliletwa katika hatua ya utendaji. Kwake ulikabidhiwa utawala juu ya vyote vilivyoonekana kwa macho yake; maana "Mungu alisema, na tumafanye mtu kwa mfano wetu na kwa sura yetu; wakatale… na nchi yote pia … Mungu akaumba mtu kwa mfano wake … mwanamume na mwanamke aliwaumba." Haa inadhihirishwa wazi mwanzo au asili ya wanadamu; na kumbukumbu hii ya kimbingu imeelezwa dhahiri kiasi kwamba hakuna sababu ya kufikia hitimisho lenye makosa. Mungu alimuumba mtu kwa mfano wake mwenyewe. Hapa hakuna siri. Hakuna sababu ya kudhania kuwa mtu alibadilika polepole kimaendeleo kutoka katika aina ya chini ya wanyama au mimea. Fundisho kama hilo hudhalilisha kazi kuu ya muumbaji hadi kiwango finyu cha mtu na ufahamu wa kidunia. Watu wamedhamiria kumtenga Mungu kutoka ukuu na utawala wa ulimwengu kiasi cha kumshusha mtu chini na kumnyang'anya heshima anayostahili ya asili yake. Yeye aliyetandaza malimwengu ya nyota juu na kuweka kwa ustadi wa juu sana rangi ya maua ya kondeni, aliyejaza dunia na mbgingu kwa maajabu ya uweza wake, alipokuja kuhitimisha kazi yake ya utukufu, kumweka ambaye angesimama kama mtawala katika dunia inayopendeza, hakushindwa kuumba kiumbe kinachostahili kwa mikono iliyokipatia uhai.

Elimu ya asili ya uzao wa binadamu, kama inavyoelezwa na uvuvio, hupata mwanzo wake, siyo katika viini vinavyoendela kubadililka, wanyama wenye miili laini, na wenye miguu minne, bali kwa muumbaji mkuu. Ingawa alitengenezwa kutoka mavumbini, Adamu alikuwa "Mwana wa Mungu."

Mwanadamu angechukua mfano wa Mungu, katika umbile lake la nje na katika tabia. Kristo pekee ndiye "chapa ya nafsi yake" baba (Waebrania 1:3); lakini mtu aliumbwa kwa sura ya Mungu. Asili yake ilipatana na mapenzi ya Mungu. Akili zake zilikuwa na uwezo wa kuyafahamu mambo ya Mungu. Upendo wake ulikuwa safi; tamaa na hisia zake zilitawaliwa na kanuni. Alikuwa mtakatifu na mwenye furaha katika kuchukua mfano wa Mungu nakatika utu mkamilifu wa mapenzi yake.

Mwanadamu alipotoka mikononi mwa Muumba wake, alikuwa na umbo kubwa na mwili uliolingana vizuri. Uso wake ulibeba rangi nzuri nyekundu yenye afya na kutoa mng'ao wa nuru yauzima na furaha.

Mungu mwenyewe ndiye aliyempatia Adamu msaidizi. Alimpatia 'msaada uliomfaa' – msaidizi aliyefanana naye yule aliyestahili kuwa mwenzi wake, na ambaye angekuwa mmoja naye katika upendo na huzuni. Hawa aliumbwa kutokana na ubavu uliotoka ubavuni wa Adamu, ikiwa ni ishara kwamba Hawa hakupaswa kumtawala kama kichwa, wala Adamu

hakupaswa kumkanyaga chini kama aliye duni kwake, lakini agesimama kando yake kama aliye sawa naye na aliyepaswa kupendwa na kutunzwa naye.

Baada ya kustarehe siku ya saba, Mungu aliitakasa, au kuitenga kando, kama siku ya mapumziko kwa Mwanadamu.

Kwa kufuata mfano wa Muumbaji wake, mwadamu alipaswa kupumzika katika siku hi takatifu, ili kwamba napoziangalia mbingu na nchi, aweze kutafakari kazi kuu ya Mungu ya Uumbaji.

Yehova mkuu aliiweka misingi ya dunia; aliivika dunia yote vazi la uzuri na kuijaza kwa vitu vya kumfaa mwanadamu; Aliumba maajabu yote nchi na bahari. Katika muda wa siku sita kazi ya uumbaji ilikamilishwa. Na Mungu "alistarehe siku ya saba kutoka kazi yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa: maana katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya."Mungu alitazama kwa kuridhika na kazi yake ya mikono yake. Yote yalikuwa makamilifu, yenye kustahili kwa Muumba wao wa kimbingu, naye akapumzika, sio kama mmoja aliyechoka, lakini ni kwa kupendezwa na matokeo ya hekima na wema wake na udhihirisho wa utukufu wake.

Baada ya kustarehe siku ya saba, Mungu aliitakasa, au aliitenga kama siku ya mapumziko kwa mwanadamu. Kwa kufuata kielelezo cha Muumbaji wake, mtu alipaswa kupumzika katika siku hii takatifu, ili kwamba anapoziangalia mbingu na nchi, aweze kutafakari kazi kuu ya Mungu ya uumbaji; na kwamba anapotazama ushahidi wa hekima ya Mungu na wemna wake, moyo wake ujazwe na upendo na heshima kwa Muumba wake.

Katika Edeni, Mungu alisimamisha kumbukumbu ya kazi yake ya uumbaji, kwa kuweka mibaraka yake katika siku ya saba. Sabato ilikabidhiwa kwa Adamu, aliye baba na mwakilishi wa familia ya wanadamu. Utunzaji wake ungekuwa ni tendo la kukiri kwa shukrani, kwa upande wa wale wote ambao wangeishi juu ya uso wa dunia, kwamba Mungu ndiye Muumbaji wao na mtawala wao halali; kwamba walikuwa ni kazi ya mikono yake na walio chini ya mamlaka yake. Hivyo desturi hii ilikuwa ni ukumbusho kamili, na ilitolewa kwa watu wote. Hakukuwa na uvuli wowote ndani yake au matumizi finyu kwa watu fulani.

Mungu alion akuwa sabato ni muhimu kwa mtu, hata katika Paradiso. Alitakiwa kuweka kando mambo yake na yale yampendezayo sana kwa siku moja ya zile saba, ili apate kufakari zaidi na kwa ukamilifu kazi za Mungu na kutafakari kuhusu uweza wake na wema wake.

Alihitaji sabato ili kumkumbusha kwa dhahiri kuhusu Mungu na kuamsha shukrani kwa sababu vyote alivyovifurahia n kuvimiliki vilitoka katika mikono ya ukarimu ya Muumbaji.

Mungu anakusudia kuwa sabato ielekeze mawazo ya watu katika kutafakari kazi zake za uumbaji. Viumbe vya asili huzungumza kwa fahamu zetu kuwa kuna Mungu aliye hai, muumbaji, na mtawala mkuu wa vyote. "Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake. Mchana husemezana na mchana usiku hutolea usiku maarifa."Zaburi 19:1,2. Uzuri unaoifunika dunia ni ishara ya upendo wa Mungu. Tunaweza kuuona kwenye vilima vya milele, kwenye miti mikubwa sana, katika vikonyo na maua laini. Vyote hutueleza kumhusu Mungu. Sabato daima huelekeza kwake yeye aliyeviumba vyote, huhimiza watu kufunua kitabu kikuu cha viumbe vya asili na kutafuta humo hekima, na nguvu, na upendo wa Muumbaji.

Kwanza za kila wiki zimepewa wanadamu ili tuzifanyie kazi, kwa sababu Mungu alitumia kipindi hicho hicho cha wiki ya wanza kwa kazi ya Uumbaji. Katika siku ya saba mtu anapaswa kuweka kando kazi zake, kwa kukumbuka pumziko la Muumbaji.

Lakini dhana kwamba matukio ya wiki ya kwanza yalihitaji maelfu kwa maelfu ya miaka, hulenga moja kwa moja kwenye msingi wa amri ya nne. Humwelezea Muumba kama anayewaamuru watu kuadhimisha wiki yenye siku halisi kwa kukumbuka kipindi kirefu sana kisich **dhahiri**. Hii ni kinyume na taratibu zake za kushughulika na viumbe vyake. Hukifanya kisicho dhahiri na kilichofichika, kile ambacho yeye amekifunua wazi. Ni ukafiri katika hali yake ya kudhuru kwa siri na hivyo kuwa katika aina hatari sana; tabia yake halisi imefichika sana kiasi kwamba hushikiliwa na kufundishwa na wengi wanaodai kuiamani Biblia.

“Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.” Maana yeye alisema, ikawa; Na Yeye aliamuru, ikasimama.”Zaburi 33:6,9. Biblia haitambui miaka mingi ambayo katika hiyo dunia ilibadilika taratibu kutoka katika kitu kisichokuwa na umbo wala utaratibu. Kwa kila siku iliyofuata ya uumbaji Biblia hutangaza kuwa ilikuwa na usiku na mchana na jioni na asubuhi, kama siku nyingine zote ambazo zimefuata. Katika mwisho wa kila siku yametolewa matokeo ya kazi ya Muumbaji. Maelezo yafuatayo yametolewa mwishoni mwa kumbukumbu ya wiki ya kwanzza: “Hivi ndivyo vizazi vya mbingu na nchi zilipoumbwa.” Mwanzo 2:4. Lakini hii haitoi wazo kwamba siku za uumbaji zilikuwa tofauti na siku halisi za kawaida. Kila siku iliitwakizazi, kwa sababu katika hiyo Mungu alifanyiza au kuleta sehemu mpya ya kazi yake.

Kumekuwa na juhudi za kudumu kueleza kazi ya uumbaji kama matokeo ya nguvu za asili; na mawazo haya ya kibinadamu yanakubalika hata miongoni mwa wale wanaodai kuwa Wakristo, huku mawazo hayo yakipinga ukweli dhahiri wa Maandiko.

“Mambo ya siri ni ya BWANA, Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele.” Kumbukumbu la Torati 29:29. Jinsi Mungu alivyokamilisha kazi ya uumbaji hajawafunulia watu kamwe; sayansi ya binadamu haiwezi kuchunguza siri zake Aliye Juu. Uwezo wake wa uumbaji hauwezi kufahamika, sawa na kulivyo kuwepo kwake.

Mungu ameruhusu mwanga ufurike katika dunia hii kupitia sayansi na elimu ya sanaa; lakini wakati watu wanaodai kuwa Wanasayansi wanashughulika na mambo haya kwa mtazamo wa kibinadamu tu, kwa hakika watafikia hitimisho lenye makosa.

Wengi hufundisha kwamba mada huifadhi uwezo muhimu – kwamba nguvu fulani zimewekwa katika mada, na kuachwa kutenda kupitia nguvu za asili ndani yake; na kwamba utendaji wa asili hufanyika kulingana na sheria zilizowekwa, ambazo Mungu mwenyewe hawezi kuziingilia. Hii ni sayansi ya uongo, na haitegezwi na neno la Mungu. Asili ni mtumishi wa Muumbaji wake.

Mungu hatangui sheria zake au kutenda kinyume nazo, lakini daima huzitumia kama chombo chake. Vitu vya asili hushuhudia upeo wa juu wa akili; kuwepo, na nguvu tendaji, ifanyayo kazi ndani na kwa kupitia sheria zake. Katika viumbe vya asili daima kuna utendaji wa Baba na Mwana. Kristo anasema, “Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi.” Yohana 5:17.

Kuhusiana na dunia hii, kazi ya Mungu ya Uumbaji imemalizika. Maana "zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Waebrania 4:3. Lakini nguvu zake bado zinatumika ili kutegemeza vitu vilivyoumbwa. Siyo kwa sababu utendaji wa mtambo uliowekwa zamani na kuanzishwa ndani yake unaendelea kutenda kwa nguvu zake zilizomo ndani yake, kwamba moyo hudunda, na pumzi hufuata pumzi; lakini kila pumzi, kila mdundo wa moyo, ni ushahidi wa utunzaji ulionenea wake Yeye ambaye ndani yake "utaishi, tunakwenda na kuwa na uhai wetu." Matendo 17:28. Siyo kwa sababu ya uwezo wa asili uliomo ndani yake kwamba dunia hutoa matunda yake mwaka hadi mwaka na kuendelea na mzunguko wake kulizunguka Jua. Mkono wa Mungu huongoza sayari na kuzidumisha mahali pake katika miendo yao kiutaratibu mbinguni.

Mungu ndiye mwanzilishi wa vitu vyote. Sayansi yote ya kweli hupatana na kazi zake; elimu yote ya kweli huongoza kwenye utii kwa serikali yake. Sayansi hufunua maajabu mapya kwetu; hupanda juu, na kuvumbua vina vipya; lakini haileti chochote kutokana na utafiti wake kinachopingana na ufunuo mtakatifu. Ujinga unaweza kutafuta kuunga mkono mitazamo ya uongo kumhusu Mungu kwa kutazamisha kwa Sayansi, lakini kitabu cha viumbe vya asili na maandiko huangaziana nuru. Hivyo tunaongozwa kumpenda sana na kuwabudu muumbaji na kulitumainia neno lake kwa akili.

TANGU MWANZO WA WAKATI

> Tangia siku hiyo hadi sasa, maarifa
> ya sheria ya Mungu yamehifadhiwa duniani,
> na sabato ya amri ya nne imetunzwa.

Kabla ya anguko wazazi wetu wa kwanza waliitunza sabato, iliyokuwa imeanzishwa Edeni; na baada ya kuondolewa kwao kutoka Paradiso waliendelea kuitunza. Walikuwa wameonja matunda machungu ya kutotii, na walikuwa wamejifunza kile ambacho kilamtu anayezikanyaga amri za Mungu atajifunza sasa au baadaye – kwamba kanuni za Mungu ni takatifu na zisizobadilika, na kuwa adhabu ya uasi hakika itafikilizwa. Sabato iliheshimiwa na watoto wote wa Adamu waliodumu kumtii Mungu. Lakini Kaini na uzao wake hawakuiheshimu siku ambayo Mungu alipumzika. Walichagua muda wao wenyewe wa kufanya kazi na wa kupumzika, bila kujali amri dhahiri ya Yehova.

Ikitukuzwa kwa pumziko la Muumbaji na mbaraka wake, sabato ilitunzwa na Adamu kabla ya dhambi katika Edeni; na pia Adamu aliitunza baada yakuanguka, na akatubu, alipokuwa amefukuzwa kutoka katika shamba lake la kupendeza. Ilitunzwa na wazee wote wa Imani, tangu Habili hadi Nuhu mwenye haki, hadi Ibrahimu, hadi Yakobo. Wakati taifa teule likiwa utumwani Misri, wengi, katikati ya ibada ya sanamu iliyowazunguka pote walipoteza ufahamu wao kuhusu sheria ya Mungu; lakini Bwana alipowakomboa Israeli, Alitangaza

sheria yake katika hali ya utukufu wa kutisha kwa makutano waliokusanyika, ili wapate kuyajua mapenzi yake, na wamche na kumtii Yeye milele.

Tangia siku hiyo hata sasa, maarifa ya sheria ya Mungu yamehifadhiwa duniani, na sabato ya amri ya nne imetunzwa. Ingawa mara nyingi katikati ya mashutumu na mateso, ushuhuda wa daima umetolewa kwa umilele wa sheria ya Mungu, na wajibu mtakatifu wa sabato ya uumbaji.

Sabato, kama ukumbusho wa uwezo wa Mungu wa uumbaji, huelekeza kwake kama Muumba wa mbingu na nchi. Kwa sababu hiyo ni ushahidi wa daima wa kuwepo kwake na ukumbusho wa ukuu wake, Hekima yake, na upendo wake. Kama sabato ingalitunzwa daima, kamwe kusingekuwa na asiyeamini kuwa Mungu yupo au mwabudu sanamu.

Desturi ya sabato ni ya kale kama ilivyo dunia yenyewe. Ilitunzwa na wazee wa imani wote tangu uumbaji na kuendelea. Wakati wa utumwa kule Misri, Wasraeli walilazimishwa na watesi wao kuivunja sabato, na kwa kiwango kikubwa walipoteza ufahamu wao kuhusu utakatifu wake. Sheria ilipotangazwa pale Sinai maneno yale ya kwanza ya amri ya nne yalikuwa, “Ikumbuke siku ya sabato uitakase”yakionyesha kuwa sabato haikuanzia pale; tunarejeshwa nyuma kwa mwanzo wake hadi uumbaji. Ili kumwondolea alikusudia kuondoa kabisa ukumbusho huu mkuu. Kama watu wataongozwa kumsahau Muumba wao, hawatafanya jitihada zozote kupinga nguvu za uovu, na shetani angekuwa na hakika ya mawindo yake.

SIKU YA KUKUMBUKA

“Ee BWANA, Wewe U karibu, Na maagizo yako yote ni kweli.” Zaburi 119:151

Katika utumwa wao [Misri] Waisraeli kwa kiwango fulani walipoteza ufahamu wao wa sheria ya Mungu, nao walijitenga mbali na kanuni zake. Sabato kwa ujumla haikujaliwa, na madai ya watesi wao yalifanya utunzaji wake kuonekana usiowezekana. Lakini Musa aliwaonyesha watu wake kuwa utii kwa Mungu ulikuwa sharti la kwanza la kukombolewa; na juhudi zilizofanyika kurejesha utunzaji wa sabato zilijulikana kwa watesi wao.

Mungu aliahidi kuwa Mungu wao, kuwachukua kwake kama taifa. [Kufuatia ukombozi wao wa miujiza kutoka utumwani Misri], akiba yao ya chakula ilianza kupungua. Jinsi gani chakula kingeweza kugawiwa kwa makutano haya makubwa? Mashaka yalijaa mioyoni mwao, na hata watawala na wazee wa watu walijiunga kuwalalamikia viongozi waliowekwa na Mungu. Walikuwa bado hawajateseka kwa njaa, mahitaji yao ya muda huo walipatiwa, lakini walihofia wakati ujao. Mungu hakusahau mahitaji ya Waisraeli. Alimwambia kiongozi wao, “Mimi nitawanyeshea ninyi mvua ya mkate kutoka mbinguni.” Maelekezo yalitolewa kwamba watu waokote sehemu ya siku kila siku, na sehemu maradufu katika siku ya sita, ili utunzaji mtakatifu wa sabato upate kudumishwa.

Asubuhi kulikuwa juu ya uso wa nchi kitu kisogo kilichoviringana. Kilikuwa kama mbegu ya mtama, nyeupe. Watu waliita “mana.” Musa alisema “huu ndio mkate BWANA aliowapatia kula. Walielekezwa kukusanya Omeri kwa siku kwa kila siku kwa kila mtu [Omeri ni kama pishi moja]; na hawakupaswa kukisaza hata asubuhi. Baadhi walijaribu kukiweka hadi siku ya pili, lakini kilionekana kutofaa kwa chakula.

Siku ya sita watu walikusanya pishi mbili kwa kila mtu. “Ndilo neno alilonena BWANA, kesho ni starehe takatifu, sabato takatifu kwa BWANA; okeni mtakachooka na hicho kitakachowasalia jiwekeeni kilindwe hata asubuhi.""Walifanya hivyo na wakakuta kimebakia salama. “Musa akasema, haya kuleni hiki leo; kwa kuwa leo ni sabato ya BWANA; leo hamtakiona nje barani. Siku sita mtaokota; lakini siku ya saba ni sabato, siku hiyo hakitapatikana.” (Kutoka 16).

Kila wiki wakati wa safari yao ndefu jangwani Waisraeli walishuhudia miujiza mitatu, iliyokusudiwa kuvuta mawazo yao kuhusu utakatifu wa sabato: sehemu maradufu ya mana ilishuka siku ya sita, haikushuka mana siku ya saba, na sehemu iliyohitajika kwa siku ya sabato ililindwa ikiwa tamu na salama, wakati ilipookotwa nakutunzwa kwa siku nyingine iliharibika na kutofaa kuliwa.

Mungu alikusudia kufanya tukio la kutangaza sheria yake kuwa la utukufu wa kutisha, kwa kufuatana na hadh yake kuu. Watu walitakiwa kupata mguso kuwa chochote kilichohusiana na huduma ya Mungu lazima kichukuliwe kwa heshima kuu sana.

BWANA alimwambia Musa, “Enenda kwa watu hawa, ukawatakase leo na kesho, wakazifue nguo zao, wawe tayari kwa siku ya tatu, maana siku ya tatu BWANA atashuka katika mlima wa Sinai machoni pa watu hawa wote.” Katika kipindi hicho cha mpito wote walipaswa kutumia muda huo kwa matayarisho ya kicho ili kuhdhuria mbele za BWANA.

Matayarisho yalifanywa, kulingana na maagizo; na kwa kutii maelekezo zaidi, Musa alielekeza kuwa kizuizi kiwekwe kando ya mlima. Kama mtu alijaribu kusogelea kiasi cha kukigusa, adhabu ilikuwa ni kuuawa mara moja.

> Mungu alijidhihirisha mwenyewe,
> siyo tu katika ukuu wa kutisha wa
> mwamuzi na mtoa sheria, lakini kama
> mwangalizi mwenye huruma kwa watu wake.

Asubuhi ya siku ile yatatu, watu wote walipotazama kuelekea mlimani, kilele chake kilifunikwa nawingu zito, lililozidi kuwa jeusi na nene, lililozidi kuenea kuelekea chini hadi mlima wote ukafunikwa katika giza na utisho wa ajabu. Ndipo sauti kama ya tarumbeta ikasikika, ikawaalika watu kukutana na Mungu; na Musa akawaongoza hadi chini ya mlima. Kutoka katika giza nene kulimulika umeme dhahiri, huku ngurumo za radi zikitoa na kurudisha mwangwi katika milima iliyozunguka pale. “Mlima wa Sinai wote pia ukatoa moshi, kwa sababu BWANA alishuka katika moto … na mlima wote ukatetemeka sana.” Ilikuwa ya kutisha sana ishara ya kuwepo kwa Mungu kiasi kwamba majeshi ya Waisraeli yalitetemeka kwa hofu, ya kuanguka kifudifudi mbele za BWANA.

Sasa radi zilikoma; tarumbeta haikusikiwa tena; nchi haikutetemeka. Kulikuwa na kipindi cha kimya kizito, na ndipo sauti ya Mungu ikasikika. Alizungumza kutoka katika giza lililomzunguka, akisimama juu ya mlima, akizungukwa na kundi la malaika, Bwana alitangaza sheria yake.

Mungu alijidhihirisha mwenyewe, siyo tu katika ukuu wa kutisha wa mwamuzi na mtoa sheria, lakini kama mwangalizi mwenye huruma kwa watu wake; “Mimi ndimi BWANA Mungu wenu, niliyewatoa katik nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.” Yeye ndiye sasa alitamka sheria yake.

Kama alama ya mamlaka ya Mungu na kuweka pamoja mapenzi yake, Musa alikabidhiwa nakala ya amri kumi zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu juu ya mbao mbili za mawe, (Kumbukumbu 9:10, Kutoka 32:15,16) ili kuzihifadhi kwa utukufu hekaluni, ambalo, baada ya kujengwa, lingekuwa kituo dhahiri cha ibada ya taifa.

Sheria haikutangazwa kwa faida ya Waebrania pake yao, Mungu aliwapa heshima kwa kuwafanya waangalizi na watunzaji wa sheria yake, lakini ilipaswa kuchukuliwa kama amana takatifu kwa ulimwengu wote kwa maongozi na utawala wa wote. Amri kumi, zenye maelezo mafupi, zinazoeleweka na zenye mamlaka, zinazohusu wajibu wa mtu kwa Mungu na kwa wanadamu wenzake; na zote zimejengwa juu ya kanuni kuu ya upendo.

Sabato haikuingizwa kama desturi mpya, lakini kama iliyoanzishwa wakati wa uumbaji. Inapaswa kukumbukwa na kuadhimishwa kama ukumbusho wa kazi ya Muumbaji. Ikielekeza kwa Mungu kama aliyezifanya mbingu na nchi, inamtofautisha Mungu wa kweli na miungu yote ya uongo. Wote wanaoitunza siku ya saba huonyesha kwa tendo hili kwamba wanamwabudu Yehova. Kwa hiyo Sabato ni ishara ya utii wa mwanadamu kwa Mungu, kadr atakavyodumu kuwepo duniani mtu wa kumtumikia. Amri ya nne ndiyo pekee miongoni mwa zote kumi linapopatikana jina na cheo cha Mtoaji wa sheria. Ndiyo pekee inayoonyesha ni kwa mamlaka ya nani sheria ilitolewa. Hivi inabeba muhuri wa Mungu, ulionganishwa katika sheria yake kama ushahidi wa uthabiti wake na nguvu za kifungo chake.

Bwana alikusudia kwamba kwa kuiangalia kwa uaminifu amri ya sabato, Waisraeli wangekumbushwa daima juu ya uwajibikaji wao kwake kama Muumba na Mkombozi wao. Kama wangeitunza sabato katika roho ya kweli, ibada ya sanamu isingekuwepo; lakini kama madai ya kanuni hii ya amri kumi itawakwa kando kama isiyopaswa kushikwa, Muumbaji atasahauliwa na watu wataabudu miungu mingine.

Hakuna desturi nyingine waliyokabidhiwa Wayahudi iliyokuwa yenye kuwatofautisha sana na mataifa yaiyowazunguka kama ilivyofanya sabato. Mungu alikusudia kwamba ujtunzaji wake uwe dalili kuwa wanamwabudu. Ilikuwa iwe ishara ya kujitenga kwao na ibada ya sanamu, na ya muunganiko wao na Mungu wa kweli. Lakini ili kuitakasa Sabato, watu wenyewe wanapaswa kuwa watakatiu. Kwa njia ya imani wanapaswa kuwa washirika wa haki ya Kristo. Wakati agizo lilipotolewa kwa Waisraeli, “Ikumbuke siku ya sabato uitakase” Bwana pia aliwaambia, “Nanyi mtakuwa watu watakatifu kwangu Mimi.” Kutoka 20:8; 22:31. Ni kwa hivi tu sabato ingewatofautisha Waisraeli kama wamwabuduo Mungu.

Wayahudi walipomwacha Mungu, na kushindwa kuifanya haki ya Kristo kuwa yao kwa njia ya imani, sabato ilipoteza maana yake kwao. Shetani alikuwa anatafuta kujitukuza na kuwavuta watu mbali na Kristo, na akafanya bidii kuipotosha sabato, kwa sababu ilikuwa ni

ishara ya nguvu za Kristo. Katika wakati mmoja, kwa agizo la Bwana, nabii [Yeremia] alisimama katika mojawapo ya malango makuu ya mji na pale alisisitiza umuhimu wa kuitakasas siku ya sabato. Wenyeji wa Yerusalemu walikuwa katika hatari ya kupoteza utakatifu wa Sabato, na walionywa kwa dhati dhidi ya kufanya shughuli zao za kawaida katika siku hiyo. "Na itakuwa kama mkinisikiliza mimi kwa bidii, asema BWANA, msiingize mzigo wowote kwa malango ya mji huu siku ya sabato, bali mkiitakasa siku ya sabato, bila kufanya kazi yoyote siku hiyo, ndipo watakapoingia wafalme na wakuu kwa malango ya mji huu; wataketi katika kiti cha enzi cha Daudi… na mji huu utakaa hata milele." Yeremia 17:24, 25

Ahadi hii ya mafanikio kama zawadi ya utii iliambatana na unabii wa hukumu ya kutisha itakayoupata mji kama wakazi wake watathibitisha kutokuwa watiifu kwa Mungu na sheria yake. Kama maonyo makali ya kumtii Bwana Mungu wa baba zao na kuiheshimu siku yake ya sabato yasingetiiwa, mji na majumba yake ya kifalme yangeharibiwa kabisa kwa moto. Lakini kwa sehemu kubwa ya watu wito na kutubu na kufanya matengenezo haukujaliwa.

"Kwa hiyo akaleta juu yao mfalme wa Wakaldayo.

…Na wale waliookoka na upanga akawachukua mpaka Babeli, wakamtumikia yeye … hata kulipoingia milki ya Uajemi, ili kulitimiza neno la BWANA kwa kinywa cha nabii Yereimia …." 2 Mambo ya Nyakati 36:17, 20, 21. (Soma Yeremia 25:9-12).

Ikumbuke Siku ya Sabato

Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.
Siku sita fanya kazi utende mambo
Yako yote; lakini siku ya saba ni
Sabato ya BWANA Mungu wako:
Siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe,
Wala mwana wako, wala binti yako,
Walamtumwa wako, wala mjakazi
wako, wala mnyama wako wa kufuga,
wala mgeni aliye ndani ya malango
yako Maana, kwa siku sita BWANA alifanya
mbingu, na nchi, na bahari na vyote
vilivyomo, akastarehe siku ya saba;
kwa hiyo BWANA akaibarikia siku
ya sabato akaitakasa.

KUTOKA 20:8-11

Naye akaja Nazareti

Nazareti, Mnamo 15AD

Tunaona duka la fundi Seremela kando ya barabara ya vumbi kuelekea ukingoni mwa mji – duka ambalo kwa wiki yote hujishughulisha na utengenezaji kwa utaratibu na wa kufaa wa Plau, nira, meza, viti na vifaa vingine vya mbao vilivyotengenezwa kwa matumizi ya shambani na nyumbani. Ijapokuwa lilijengwa uchochoroni, bila shaka ilikuwa karakana bora katika Palestina yote, kwa kuwa Yeye aliyebuni na kuutengeneza ulimwengu anafanya kazi pale, ingawa hakujitambulisha kwa waliokuwepo. Mara chache tu hakuna kazi. Kuanzia siku ya kwanza ya juma na kuendelea, wateja wanaonekana wakiingia na kutoka dukani. Wengi wao walitegemea ukarabati wa vifaa vya kilimo vilivyoharibika na utengenezaji wa vifaa vipya kwa ajili ya kujipatia riziki. Mara nyingi usiku uliingia kabla mtu hajasikia pigo la mwisho la msumeno, nyundo na randa katika duka hili nyenyekevu katika Nazareti.

Lakini lo, ni nini tunachoona katika siku ya sita ya wiki? Kazi zinasimama mchana. Duka linafagiliwa kwa uangalifu na kusafishwa; zana za kazi zinawekwa mahali panapostahili kutunzia. Mwanzo tu wa alasiri duka liko tupu na tulivu, maana sabato inakaribia, na hii ni siku ya maandalio. Familia ya Yusufu inafanya kazi kwa uchangamfu na juhudi kuandaa nyumba yao kwa ajili ya siku takatifu ya Mungu waliyokaribisha daima.

Kwa utulivu jua likielekea upeo wa magharibi, juu linasambaza mionzi yake ya dhahabu kwa joto tele juu ya vilima vyenye kijani kibichi na mabonde. Vivuli vinarefuka kadri siku ilivyofifia kuelekea rangi ya zambarau ya giza la jioni. Baada ya mchana watu wameendelea kupungua mitaani. Wachungaji na wakulima wamerudi mapema kutoka mashambani. Hata watoto wanaacha michezo yao kabla ya jua kuzama.

> Bwana wa Sabato, amejaa neema na kweli, alikuja kuanzisha pumziko la sabato muhimu sana kwa urejeshwaji wa wanadamu kupitia Injili ya milele.

Mlio mkali wenye kuashiria wa pembe ya kondoo dume ulipenya anga tulivu la jioni, ili kusalimu kukaribia kwa masaa matakatifu. Mara baadaye nyimbo zinasikika kila nyumba. Nyimbo zenye mvuto na hamu za Sayuni, za kutamani Paradiso, ziliikaribisha Sabato. Taaa zinawashwa na nuru ya sherehe takatifu, yenye kumbukumbu kidogo ya kupendeza maishani, ikichezas katika kila jicho.

Mazungumzo yalieleka masomo ya mbinguni wakati wa chakula cha familia. Matajiri na maskini wako huru na masumbufu yao ya kila wiki kwa siku nyingine yenye baraka ya Sabato. Mungu anakaribia kwa upendo kuwasiliana na watoto wake katika hema hii takatifu ya wakati. Jioni inakuwa usiku, na wote kwa furaha wanakwenda kulala, kwani mizigo ya wiki imewekwa kando, na masumbufu yote yamekabidhiwa kwake awezaye kuwatunza watu wake. (Zaburi 55:22).

Asubuhi inayofuata duka la Seremela linabakia limefungwa. Hakuna mteja anayeujaribu mlango au kuutupia jicho zaidi ya mara moja, kadri watu wa mji, kutoka majumbani na vibandani mwao wote wakielekea kutoka majumbani na vibandani mwao wote wakielekea kwenye masinagogi kwa miguu. Yesu na familia yake wanaenda pia.

Nazareti: 27 AD

Miaka kadhaa baadaye kijana mwenye uso wa rangi ya shaba, mwenye uso uliozoeleka, wa amani anajiunga nakundi la wanaoabudu katika njia hii inayopitika mara kwa mara. "Naye akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome. Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa, Roho wa Bwana yu yangu, kwa maana amenitia mafuta kwahaubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru walioteswa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa … Akaanza kuwaambia, leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu. Wakamshuhudia wote wakiyastaajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani mwake." Luka 4:16-19, 21, 22.

Bwana wa Sabato, amejaa neema na kweli, alikuja kuanzisha pumziko muhimu sana la sabato kwa urejeshwaji wa wanadamu kupitia injili ya milele. Katika maisha na mafundisho yake aliikuza sheria na kuitukuza, bila lawama akazitunza amri zote za Baba yake; na kwa kafara yake alifanya haki yake izunguke kama kijitochenye nguvu kutoka Kalwari hadi katika kila moyo uliotayari. Pia alikabidhi roho Mtakatifu ili kuwaongoza wafuasi wake kwenye kweli yote, na kasema, "Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo." Yohana 13:15. Kristo aliyonyesha jinsi ya kutunza sabato, iliyo ishara kuu ya uumbaji wake, kuwa takatifu. Naye aliwafundisha wanafunzi wake, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu." Yohana 14:15. Katika uhai wake na kifo chake aliitunza sabato (Luka 23:50-56). "Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu" Waebrania 4:9.

Na Brian Jones

Shofari ni pembe ya Kondoo dume iliyopigwa na kuhani wa Kiyahudi. Bado inatumika katika Masinagogi ya Waothordox leo.

KUTOKA HUZUNI HADI FURAHA

Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao
Na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. (Mathayo 11:28)

Wayahudi walipomwacha Mungu, na kushindwa kuifanya haki ya Kristo kuwa yao kwa njia ya imani, sabato ilipoteza umuhimu wake kwao. Katika siku za Kristo Sabato ilikuwa imepotoshwa sana hadi utunzaji wake ukawa unaonyesha tabia ya wanadau ya ubinafsi na ushupavu badala ya tabia ya upendo ya Baba wa mbinguni. Kwa kweli Marabi walimwakilisha Mungu kama atoaye sheria ambazo haikuwezekana watu kuzitii. Waliongoza watu kumtakazama Mungu kama mtawala mkandamizaji na kufikiri kwamba utunzaji wa sabato, kama alivyohitaji, uliwafanya watu kuwa na mioyo migumu na wakatili. Ilikuwa kazi ya Kristo kuondolea mbali kutofahamu huko. Ingawaje Marabi walimfuata kwa uadui usio na rehema, Hakuonekana kujali hata kufuata matakwa yao, lakini aliendelea mbele, akiitunza sabato kulingana na sheria ya Mungu.

Katika siku moja ya sabato, Mwokozi na wanafunzi wake walipokuwa wakirudi kutoka mahali pa ibada, walipita katikati ya shamba lililokuwa nanafaka iliyokuwa inapevuka. Yesu alikuwa ameendelea na kazi yake zaidi ya muda wa kawaida, na walipokuwa wakipita shambani, wanafunzi wake walianza kukusanya masuke, na kuanza kula viini vyake baada ya kuyasugua.

Katika siku nyingine ya kawaida kitendo hiki kisingeamsha maoni yoyote, kwani mtu aliyepita katikati ya shamba la nafaka, miti ya matunda, au mizabibu, alikuwa huru kukusanya kiasi alichohitaji kula. (Tazama Kumbukumbu la Torati 23:24,25). Lakini kufanya hivyo siku ya sabato lilichukuliwa kuwa tendo la kunajisi. Siyo tu kwamba kuvunja masuke ilikuwa aina ya uvunjaji, lakini kuzisugua mikononi kulikuwa namna ya Kupura. Hivyo, kwa maoni ya Marabi, kulikuwa na makosa mawili.

Aliposhutumiwa kuivunja sabato kule Bethsaida, Yesu alijitetea kwa kuthibitisha kuwa ni Mwana wa Mungu, na kutangaza kwamba alifanya kazi kwa kupatana na Baba yake. Sassa kwamba wanafunzi wanashambuliwa, alitaja kwa washitaki wake mfano kutoka Agano la kale, matendo yaliyofanyika siku ya sabato na wale waliomtumikia Bwana. "Hamkusoma alivyotenda Daudi, alipokuwa na njaa, yeye na wenziwe? Jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu, akaila mikate ile ya wonyesho, ambayo si halali kuila … ila kwa makuhani peke yao?" "Akamwambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato." "Wala hamkusoma katika torati, kwamba siku ya Sabato makuhani hekaluni huinajisi sabato wasipate hatia? Lakini nawaambieni kwamba, hapa yupo aliye mkuu kuliko hekalu." Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato pia." Luka 6:3,4; Marko 2:27, 28; Mathayo 12:5,6.

Mwanafunzi, kwa kuifanya kazi ya Kristo, walikuwa katika kazi ya Mungu, na kile kilichokuwa muhimu ili kukamilisha kazi hii, kilikuwa ni halali kufanyika siku ya sabato.

Wanafunzi, katika kufanya kazi ya risto, walikuwa katika kazi ya Mungu, na kile kilichokuwa muhimu ili kukamilisha kazi hii, kilikuwa ni halali kufanyika siku ya sabato.

Kristo aliwafundisha wanafunzi wake na maadui zake kuwa kazi ya Mungu inapaswa kuwa ya kwanza kwa zote. Lengo la kazi ya Mungu hapa duniani ni kwa vile alifanya vitu vyote, Aliifanya pia Sabato. Ni Yeye aliitenga kama kumbukumbu ya kazi ya uumbaji. Inaelekeza kwake kama Muumbaji na Atakasaye, Sabato ni ishara ya uwezo wa Kristo kutufanya Watakatifu. Ukombozi wa Mwanadamu; kwahiyo kile kilicho muhimu kufanyika siku ya sabato ili kukamilisha kazi hii kinapatana na sheria ya Sabato. Yesu akahitimisha hoja yake kwa kujitangaza Mwenyewe kuwa "Bwana wa Sabato"- Yeye aliye juu ya maswali yote na sheria yote. Mwamuzi huyu mkuu asiye na mwisho anatangaza kuwa wanafunzi hawana hatia dhidi ya shutuma hizo, akiwatazamisha kwenye amri ile walioashutumiwa kuivunja.

Yesu hakuachia swala hili kupita pasipo kutoa karipio kwa maadui zake. Alisema kwamba katika upofu wao walikuwa wamekosea kusudio la sabato. Alisema, "kama mngalijua maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka, msigaliwalaumu wasio na hatia." Mathayo 12:7.

Katika siku nyingine ya Sabato, Yesu alipoingia katika sinagogi, Alimwona mtu mwenye mkono uliopooza. Mafarisayo walimwangalia kwa makini, wakiwa na shauku ya kuona kile atakachofanya. Mwokozi alijua vizuri kwamba kwa kuponya siku ya sabato angechukuliwa kama mvunja sheria, lakini hakusita kuangusha ukuta wa matakwa ya mapokea yaliyoizunguka sabato. Yesu alimwambia mwenye kupooza asimame, kisha akawauliza, Je, ni halali kutenda mema siku ya sabato, au kutenda mabaya? Kuokoa maisha au kuangamiza? "Ilikuwa ni kanuni miongoni mwa Wayahudi kwamba kushindwa kutenda jema, wakati mtu amepata nafasi hiyo, ilikuwa kutenda dhambi; kutojali kuokoa maisha ilikuwa uuaji. Kwa hiyo, Yesu aliwakabili kanuni yao wenyewe. "Wakanyamaza. Akawakazia macho pande

zote kwa hasira, akiona huzuni kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao, akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako. Naye akaunyosha; mkono wake ukawa mzima tena." Marko 3:4, 5.

Kwa kuuponya mkono uliopooza, Yesu alihukumu desturi ya Kiyahudi kuwa na hatia, na kuiacha amri ya Mungu ya nne kubakia vile vile kama ilivyoamriwa. "Ni halali kutenda mema siku isiyo ya busara ya kiyahudi, Kristo aliitukuza sabato, huku wale waliomshutumu wakiwa hawaisheshimu siku takatifu ya Mungu.

Wale wanaoshikilia kuwa Krsto aliondoa sheria hufundisha kwamba Aliivunja sabato na kukubaliana na kitendo cha wanafunzi wake kufanya hivyo. Hivyo wanasimama sawa na Wayahudi walioweka makatazo hafifu. Katika hili wanapingana na ushuhuda wa Kristo mwenyewe, aliyesema, "Mimi nimezishika amri za Baba yangu na kukaa katika Pendo lake." Yohana 15:10. Si mwokozi wala wanafunzi wake walivunja sheria ya sabato. Kristo ni kielelezo hai cha sheria. Hakuna uvunjaji wowote wa kanuni zake takatifu ulioonekana ndani yake.

"Basi, Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato pia." Maneno haya yamejaa mafundisho na faraja. Kwa sababu Sabato ilifanyika kwa ajili ya Mwanadamu, hiyo ndiyo siku ya Bwana. Ni mali ya Kristo. Kwani vitu vyote vilifanyika na Yeye; na pasipo Yeye hakukuwa na chochote kilichofanyika." Yohana 1:3. Kwa kuwa aliviumba vitu vyote, aliiumba Sabato. Ni Yeye aliitenga Sabato kuwa ukumbusho wa kazi yake ya uumbaji. Huelekeza kwake kama muuombaji na Mtakasaji. Sabato ni ishara ya uwezo wa Kristo kututakasa na kutufanya watakatifu. Na imetolewa kwa wote anaowatakasa Kristo. Kama ishara ya uwezo wake wa kutakasa, sabato imetolewa kwa wote ambao kupitia Kristo hufanyika kuwa sehemu ya Israeli wa Mungu.

Kwa wote wanoipokea Sabato kama ishara ya uwezo wa Kristo wa kuumba na kukomboa, itakuwa ni siku ya furaha. Wakimwona Kristo katika Sabato, hupendezwa katika Yeye. Sabato huwaelekeza katika kazi za Uumbaji kama ushahidi wa uwezo wake mkuu wa ukombozi. Huku ikikumbusha amani iliyotoweka ya Edeni, huelezea amani iliyorejeshwa kupitia kwa mwokozi. Na kila kitu cha asili hurudia mwaliko wake, "Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo nami nitawapumzisha." Mathayo 11:28.

Kristo alimaliza kazi aliyokabidhiwa kuifanya. Alikuwa amemtukuza Mungu duniani. Alilijulisha jina la Baba. Alikuwa amwakusanya wale ambao wangendeleza kazi yake miongoni mwa mwatu.

Mwana wa Mungu asiye na doa aliwambwa msalabani, nyama ya mwili wake ikiwa imeharibiwa kwa mijeledi, mikono ile iliyonyooshwa mara nyingi ili kubariki, ilikuwa imepigiliwa misumari kwenye mti; miguu ile ambayo haikuchoka kwa huduma za upendo ilipigiliwa misumari katika mtu; kichwa cha kifalme kilikuwa kimechomwa kwa taji ya miiba; midomo ile iliyotetemeka ikiwa katika hali ya kulia ole, na yote aliystahimili, - jasho la damu lililotiririka usoni, mikono yake, miguu yake, maumivu makali yaliyoshtua mwili wake, na uchungu mkali usioelezeka ulioipata roho yake wakati Baba alipoficha uso wake, - hunena na kila mwanadamu, ikitangaza, kuwa, "Ni kwa ajili yako kwamba Mwana wa Mungu alikubali kubeba mzigo huu wa hatia; kwa ajili yako anaharibu utawala wa mauti, na kufungua milango ya Paradiso." Yeye aliyetuliza bahari iliyochafuka, aliyewafanya. Pepo (mashetani) kutetemeka na magonjwa kukimbia, aliyefumbua macho ya vipofu, na kuwafufua wafu, - anajitoa mwenyewe msalabani kuwa kafara, na hii ni kutokana na upendo

wake kwako. Yeye, mbeba-dhambi, anastahimili hasira ghadhabu ya haki ya Mungu, na kwa ajili yako anafanywa kuwa dhambi.

Kristo hakutoa uhai wake hadi alipokamilisha kazi aliyokuja kuifanya, na wakati alipokaribia kutaka roho alisema, "Imekwisha." Yohana 19:30. Alikuwa ameshinda vita.

Kwa taratibu na kicho Yusufu na nikodemo kwa mikono yao wenyewe waliuondoa mwili wa Yesu Msalabani. Machozi yao ya huruma yalidondoka kwa haraka walipoutazama mwili wake uliojeruhiwa na kuchukuliwa.

Yusufu alimiliki kaburi jipya, lililochongwa kwenye mwamba. Pale wanafunzi watatu [Petro, Yakobo na Yohana] waliinyosha miguu iliyopinda na kukunja mikono iliyochubuliwa kifuani. Wanawake kutoka Galilaya walikuja kuhakikisha kuwa kila kilichopaswa kufanyika kwa ajili ya mwili wa mwalimu wao mpendwa aliyekufa, kimefanyika. Halafu wakaona jiwe zito likivingirishwa kufunga mlango wa kaburi, na mwokozi aliachwa amepumzika. "Nao wakarudi … na sabato wakastarehe kama ilivyoamriwa." Luka 23:56

YESU KABURINI

Hatimaye Yesu alipumzika. Siku ndefu ya aibu na mateso ilifikia mwisho wake. Mionzi ya mwisho ya jua lililokuwa linakuchwa ikaribisha sabato, Mwana wa Mungu alilala kimya katika kaburi la Yusufu. Kazi yake ilimalizika, mikono yake ikakunjwa kwa amani, alipumzika katika masaa matakatifu yasiku ya sabato.

Hapo mwanzo Baba na Mwana walipumzika siku ya sabato baada ya kazi yao ya uumbaji. Sasa Yesu alipumzika kwa kazi ya ukombozi, ingawa kulikuwa na majonzi kwa wale waliompenda duniani, mbinguni kulikuwepo furaha. Ahadi ya wakati ujao ilikuwa yenye utukufu kwa viumbe vya mbinguni. Uumbaji uliorejeshwa, taifa lililokombolewa, ambalo baada ya kushinda dhambi lisingeweza kuanguka tena – hili, likiwa matokeo ya kazi Kristo aliyoikamilisha, Mungu na Malaika waliiona. Pamoja na tuko hili siku ile Yesu alipopumzika imefungamanishwa milele. Maana "Kazi zake ni kamilifu," na lolote Mungu alitendalo, litadumu milele." Kumbukumbu 32:4; Mhubiri 3:14. Wakati wa "zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha Manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa Ulimwengu." Matendo 3:21, Sabato ya uimbaji, siku ambayo Yesu alipumzika katika kaburi la Yusufu, itaendelea kuwa siku ya kustarehe na kufuruahia. Mbingu na nchi zitaungana katika kusifu, vile "Sabato hata Sabato" (Isaya 66:23) mataifa ya waliokombolewa watakaposujudu katika ibada ya furaha kwa Mungu na Mwanakondoo.

Usiku wa siku ya kwanza juma ulitoweka taratibu. Jiwe kubwa lilikuwa kwenye mlango wa kaburi; muhuri wa Kirumi haukuharibiwa; Maaskari wa Kirumi walishika zamu zao.

"Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la nchi, kwa sababu Malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni."

Nchi inatetemeka napokaribia, majeshi ya giza yanakimbia, na anapoliondoa jiwe, mbingu zinaonekana kushuka chini. Maaskari wanamwona akiliondoa jiwe kana kwamba anaondoa changarawe, na wamamsikia akilia kwa sauti, "Mwana wa Mungu, njoo huku nje; Baba yako anakuita." Wanamwona Yesu akitoka kaburini, na wanamsikia akitangaza juu ya kaburi lililopasuliwa, "Mimi ndimi ufufuo na uzima."

Wanawake waliosimama kando ya msalaba wa Kristo walingoja na kukesha kusubiri masaa ya Sabato yapita. Katika siku ya kwanza ya juma, alfajiri na mapema, waliondoka kwenda kaburini, wakichukua pamoja nao manukato ili kuupaka mwili wa mwokozi.

Wakiwa hawajui hata lililokuwa linatokea muda huo, waliikaribia bustani lilimokuwa kaburi wakisema "Ni nani atakayetuondolea jiwe kaburini?" Walifahamu kwamba wasingeweza kuliondoa jiwe, lakini hata hivyo waliendela mbele. Ghafla, mbingu zinang'aa kwa utukufu ambao haukutokana na mwanga wa jua lililochomoza. Nchi ikatetemeka. Waliona kuwa jiwe lile kubwa lilikuwa limeondolewa. Na kaburi
Lilikuwa tupu.

Nuru iliangaza pale kaburini, lakini mwili wa Yesu haukuwemo. Walipokawia pale kaburini, mara waligundua kuwa hawakuwa peke yao. Kijana aliyevaa nguo zilizong'aa alikuwa amekaa pale kaburini. Ni yule malaika aliyekuwa ameliondoa jiwe.

Waligeuka ili wakimbie, lakini maneno ya malaika yalizuia hatua zao. "Msiogope," alisema kwani najua kuwa mnamtafuta Yesu, Aliyesulibiwa. Hayupo hapa; kwa kuwa amefufuka, kama alivyosema. Njoni, mpaone mahali Bwana alipolala. Nendeni upesi, na kuwaambia wanafunzi wake kuwa amefufuka katika wafu."

Msilitazame kaburi lililo tupu. Yesu yu hai, na kwa sababu yu hai, nasi pia tutakuwa hai. Amini, nawe uatauona utukufu wa Mungu. (Math. 28, Marko 16, Lk.24, Yoh.20)

MAWINGI KATIKA MSTARI WA UPEO WA MACHO.

Wana amani nyingi waipendao sheria yako; wala hawana la kuwakwaza.

ZABURI 119:165

Kanisa ndilo wakala wa Mungu kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Lilianzishwa kwa ajili ya huduma, na utume wake ni kupeleka injili ulimwenguni.

Agizo la Injili ni mkataba mkuu wa umishenari wa ufalme wa Kristo. Wanafunzi walipaswa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya roho zas watu. Walipaswa kwenda kwa watu na ujumbe wao. Kila neno na tendo lao lilitakiwa kukaza mawazo yao katika jina lake, kama lenye ile nguvuinayotakiwa ili mwenye dhambi aokolewe. Jina la Kristo lilipaswa kuwa alama ya kuwatofautisha, mamlaka kwa ajili ya kutenda kwao, na chanzo cha mafanikio yao.

Kule Troa, kandokando ya bahari ya shamu, Paulo aliona maono wakati wa usiku; alimwona mtu amesimama kutoka Makedonia, akimsihi na kusema, Vuka uje Makedonia, utusaidie."

"Baada ya kupata yale maono"anasema Luka, yeye aliyeambatana na Paulo na sila na Timotheo katika safari yao katika ulaya "mara tukataka kutoka kwenda … tukafika Filipi, mji

ulio mkuu katika jimbo lile la Makedonia, mahali walipohamia Warumi … Hata siku ya Sabato," Luka anaendelea kusema, "tukatoka nje ya lango, tukaenda kando yamto, ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali; tukaketi, tukasema na wanawake waliokutana pale. Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau … mcha Mungu, akatusikiliza; ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo." Lidia aliupokea ukweli kwa furaha. Yeye na nyumba yake wakaongoka na kubatizwa. (soma Mdo 16:11-40)

Baada ya kutoka Filipi, Paulo na Sila walielekea Thesalonike. Hapa walipata nafasi ya kuhutubia watu wengi katika Sinagogi la Wayahudi. Kwa Sabato tatu mfululizo Paulo aliwahuribiria Wathesalonike, akahojiana nao katika Maandiko kuhusu uzima, mauti, ufufuo, na ufukufu ujao wa Kristo.

Ilikuwa siku ya Sabato Bwana wa utukufu alipomtokea mtume aliyekuwa uhamishoni (Yohana). Sabato ilitunzwa kuwa takatifu na Yohana kisiwani Pattmo sawa na alipohubiri watu katika miji mikubwa na midogo katika Uyahudi. Alidai kuwa yake, mibaraka ya thamani iliyotolewa kuhusu siku hiyo. "Nalikuwa katika roho, siku ya Bwana," anaandika Yohana.

Katika karne za kwanza sabato ya kweli ilitunzwa na Wakristo wote. Walikuwa na wivu kwa ajili ya heshima au utukufu wa Mungu, na wakiamini kwamba sheria yake haibadiliki, kwa bidii waliheshimu kanuni zake takatifu. Lakini kwa kila hila kubwa, shetani alitenda kupitia mawakala wake ili kutimiza lengo lake. Ili mawazo ya watu yaelekezwe Jumapili; ilifanywa kuwa siku ya kuadhimisha ufufuo wa Kristo. Huduma za kidini zilifanyika siku hiyo;

Mfalme Constantino alitoa amri ya kuifanya Jumapili kuwa sikukuu ya Kitaifa katika himaya yote ya Kirumi. Siku ya jua iliheshimiwa sana na manaibu wake wapagani, na kuheshimiwa na Wakristo.

Hata hivyo bado ilichukuliwa kama siku ya maburudisho, hali Sabato ikiendela kutunzwa kuwa takatifu. Ili kuandaa njia kwa kazi aliyokusudia kuikamilisha, Shetani aliwaongoza Wayahudi, kabla yakuja Kristo kuibebesha Sabato mizigo kwa masharti mengi magumu, na kufanya utunzaji wake kuwa mzigo. Sasa kwa kutumia nafasi hiyo ya nuru potofu, aliyokuwa ameifanya Sabato kuchukuliwa au kueleweka hivyo, aliweka dharau juu ya sabato kama desturi ya Kiyahudi. Huku Wakristo wakiendelea kuadhimisha Jumapili kama sikukuu ya furaha, aliwaongoza, ili kuonyesha chuki yao dhidi ya dini ya Kiyahudi, kuifanya sabato kuwa saumu, siku ya huzuni na Utusitusi.

Mwanzoni mwa karne ya nne, mfalme Constantino alitoa amri ya kuifanya Jumapili kuwa sikukuu ya kitaifa katika himaya yote ya Kirumi. Siku ya jua iliheshimiwa sana na manaibu wake wapagani na kuheshimiwa na Wakristo, ilikuwa ni sera ya mfalme huyu kuunganisha mapenzi yaliyopingana ya Upagani na Ukristo. Alihimizwa kufanya hivyo na kasisi wa kanisa, ambaye kwa kuchochewa na tamaa na kiu ya madaraka, alihisi kwamba kama siku moja tu ingeadhimishwa na Wakristo na Wapagani, itahamasisha wapagani kuukubali Ukristo kwa jina tu, na hivyo kuendeleza mamlaka na utukufu wa kanisa. Lakini wakati wacha Mungu wengi katika Ukristo walifanywa kuiheshimu Jumapili kuwa na kiwango fulani cha utakatifu, bado waliishika Sabato ya kweli kuwa takatifu kwa Bwana, na waliiadhimisha katika kutii amri ya nne.

Mdanganyifu mkuu hakuwa amemaliza kazi yake. Alinuia kuwakusanya Wakristo wote chini ya bendera yake, na kutumia uwezo wake kupitia kwa kaimu wake, askofu mkuu mwenye kiburi aliyedai kuwa mwakilishi wa Kristo. Kwa kupitia wapagani walioongoka nusunusu, maaskofu wenye tamaa na waumini walioupenda ulimwengu, alitimiza kusudio lake. Mabaraza makubwa mno yalifanyika mara kwa mara, ambamo viongozi wakuu wa makanisa walikusanyika kutoka duniani kote. Karibu katika kila baraza sabato iliyowekwa na Mungu alizidi kukandamizwa chini zaidi, huku Jumapili ikizidi kutukuzwa. Kwa hivyo sikukuu hii ya kipagani hatimaye ikaheshimiwa kama desturi takatifu, huku sabato ya Biblia ikitangazwa kuwa mapokeo ya dini ya Kiyahudi (Judaism), na utunzaji wake ulitangazwa kwamba umelaaniwa.

"Nalikuwa katika Roho siku ya Bwana," "siku ya saba ni Sabato ya Bwana."
Ufunuo 1:10, Kutoka 20:10

Mwasi mkuu alifanikiwa kujitukuza "juu ya kila kiitwacho Mungu, ama kuabudiwa." (Soma 2Wathesalonike 2:4). Alithubutu kubadili kanuni pekee ya sheria takatifu ambayo kwa hakika huwaelekeza watu wote kwa Mungu wa kweli aliye hai. Katika amri ya nne Mungu anadhihirishwa kama Muumbaji wa mbingu na nchi, na hivyo kutofautishwa na miungu yote ya uongo.

Katikati ya giza lililofunika dunia katika kipindi kirefu cha utawala wa Papa, nuru ya kweli kamwe haikutoweka Mungu, - watu walioshikilia imani katika Kristo kama mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu, walioichukulia Biblia kama kanuni pekee ya maisha, na kuitukuza sabato ya kweli. Walipachikwa jina la wazushi, makusudi yao yalitiliwa mashaka, tabia zao, zilichongewa, maandiko yao yakakandamizwa, kupotosha au kuharibiwa. Hata hivyo walisimama imara, na toka kizazi hadi kizazi walidumisha imani yao katika usafi wake, kama urithi mtakatifu kwa vizazi vijavyo.

Katika nchi zisizokuwa chini ya mamlaka ya Rumi, kwa karne nyingi kulikuwa na makundi ya Wakristo waliobaki bila kuchafuliwa na uchafu wa (Rumi) Papa. Walizungukwa na upagani, na baada ya kupita miaka kadhaa, wakaathirika na makosa yake; lakini waliendelea kuheshimu Biblia kama mwongozo pekee wa imani, na kushikilia kweli zake nyingi. Wakristo hawa waliamini katika umilele wa sheria ya Mungu, nao waliitunza sabato ya amri ya nne. Makanisa yaliyoshikilia imani na desturi hii, yalikuwa katika Afrika ya kati na miongoni mwa Waarmenia wa Asia.

Lakini kati ya wale waliopinga kuingiliwa na mamlaka kuu ya Upapa, Waldensia walikuwa mstari wa mbele. Katika nchi ambayo Upapa ulikuwa umeweka kiti chake, hapo uwongo na uchafu wake ulipingwa vikali.

Miongoni mwa sababu za mbele zilizopelekea kujitenga kwa kanisa la kweli kutoka Rumi, ilikuwa ni chuki ya Rumi kwa Sabato ya Biblia. Kama ilivyotabiriwa, mamlaka ya Upapa iliangusha kweli hadi chini. Sheria ya Mungu ilikanyagwa chini, huku mila na desturi za wadamu zikitukuzwa. Makanisa yaliyokuwa chini ya mamlka ya Papa yalilazimishwa mapema kuiheshimu Jumapili kama siku takatifu. Kati ya kuenea kwa makosa na imani ya roho, wengi, hata miongoni mwa watu wa

“Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu.” Matendo 17:2

kweli wa Mungu, walichanganyikiwa sana, kiasi kwamba licha ya kuitunza sabato, pia hawakuwa wakifanya kazi siku za Jumapili. Lakini hili halikuwaridhisha viongozi wa Upapa. Walidai kwamba Jumapili isitukuzwe tu, bali pia sabato inajisiwe; nao waliwalaani kwa maneno makali wale waliothubutu kuiheshimu. Ilibidi tu kuukimbia utawala wa Rumi ili mtu yeyote aweze kutii sheria ya Mungu kwa amani.

Mamia ya miaka kabla ya matengenezo [Waldensia] walikuwa na maandishi ya mkono ya Biblia katika lugha ya wenyewe. Walikuwa na ukweli usioghasiwa, na hili liliwafanya kuwa lengo maalum la chuki na mateso. Walionyesha kuwa kanisa la Rumi ndilo Babeli mwasi wa kitabu cha Ufunuo, na kwa kuhatarisha maisha yao walisimama kupinga uovu wake … Katika miaka yote ya giza na uasi, kulikuwa na Waldensia waliokataa utawala wa Rumi, waliokataaa kusujudia sanamu kama ibada ya sanamu, na waliotunza sabato ya kweli.

Lakini Ombeni ili
Kukimbia kwenu
Kusiwe wakati wa
Baridi, wala siku
Ya Sabato

MATHAYO 24:20

“Oka akamkasirikia yule
Mwanamke, akaenda zake afanye
Vita juu ya wazao wake walioasalia
Wazishikao amri za Mungu, na
Kuwa na ushuhuda wa Yesu.”

UFUNUO 12:17

Katika Mazingiwa

Katika vita vitakavyopiganwa katika siku za mwisho kutakuwa na muungano dhidi ya watu wa Mungu, wa mamlaka zote za uovu ambazo zimeasi na kutotii sheria ya Yehova. Katika pigano hili sabato ya amri ya nne itakuwa kiini kikuu cha jambo lenyewe, kwani katika amri ya nne mtoaji mkuu wa sheria anajithibitisha kuwa muumbaji wa mbingu na nchi.

Sabato itakuwa kipimo kikuu cha utii, kwani ndiyo kiini cha ukweli hasa unaoshindaniwa. Wakati jaribu la mwisho litakapokuja juu ya wanadamu, ndipo mstari wa kutenganisha utakapochorwa kati ya wale wanaomtumikia Mungu na wale wasiomtumikia. Huku utunzaji wa sabato ya uongo kwa kupatana na sheria ya nchi, kinyume na amri ya nne, itakuwa ni kuthibisha wazi utii kwa mamlaka inayopingana na Mungu, utunzaji wa sabato ya kweli, katika kutii sheria ya Mungu, ni ushahidi wa utii kwa muumbaji. Wakati kundi moja, kwa

kuikubali ishara ya utii kwa mamlaka ya kidunia, wataipokea alama ya mnyama, kundi jingine, likichagua ishara ya utii kwa mamlaka ya Mungu, watapokea muhuri wa Mungu.

Sabato itakuwa
Ndiyo kipimo kikuu cha utii,
Kwani ndiyo kiini cha
Ukweli hasa unaoshindaniwa

Kwa kuwa sabato imekuwa kiini maalum cha mashindano katika Ukristo, na mamlaka za kidini na serikali zimeungana kulazimisha utunzaji wa Jumapili, kuendelea kwa kundi dogo kukata kuridhia madai ya watu wengi kutawafanya kuwa lengo la maangamizi kiulimwengu. Itadaiwa kwamba hawa watu wachache wanaopinga desturi ya kanisa na sheria ya nchi hawapaswi kuvumiliwa; na kwamba ni bora wao wateseke kuliko mataifa yote kuingia kwenye machafuko na kutotii sheria.

Viongozi wa kanisa na wa nchi wataungana ili kutoa rushwa, kushawishi, au kulazimisha makundi yote kuiheshimu Jumapili. Upungufu wa mamlaka ya kimbingu wa ibada hii, utajazilizwa kwa sheria za ukandamizaji.

Wakristo wa vizazi vilivyoripita waliiheshimu Jumapili, wakidhani kwamba kwa kufanya hivyo walikuwa wakiishika Sabato ya Biblia; na hata sasa wako Wakristo wa kweli katika kila kanisa, bila kuondoa ushirika wa kanisa Katoliki la Roma, ambao kwa unyofu wanaamini kwamba Jumapili ni Sabato iliyowekwa na Mungu. Mungu anaukubali unyofu wao na uaminifu wao kwake. Lakini wakati utunzaji wa Jumapili utakapolazimishwa kwa sheria, na ulimwengu kuangaziwa kuhusu wajibu wa kuitunza sabato ya kweli, ndipo yeyote atakayeasi amri ya Mungu, ili kutii kanuni isiyo na mamlaka ya juu zaidi ya yale ya Rumi, kwa njia hiyo atakuwa anauheshimu Upapa kuliko Mungu. Atakuwa anaonyesha utii wake kwa rumi na kwa mamlaka inayolazimisha desturi iliyoanzishwa na Rumi. Atakuwa anamsujudia mnyama na sanamu yake. Wakati watu watakapokataa desturi ambayo Mungu ameitangaza kuwa ishara ya mamlaka yake, na badala yake kuheshimu ile iliyowekwa na Rumi kama alama ya ukuu wake, watakuwa wameipokea ishara ya uaminifu wao kwa Rumi – yaani “alama ya mnyama.” Na ni pale jambo hili litakapowekwa wazi mbele ya watu, na kutakiwa kuchagua kati ya amri za Mungu na amri za wanadamu, ndipo wale watakaondelea kuasi watapokea “alama ya mnyama.’

Katika kubadili sabato kwenda siku ya kwanza ya juma [Shetani] yeye huwaongoza watu, kutoamini tangazo la Mungu, na hivyo kuheshimu njia zao wenyewe na mipango yao kwamba wanajiona wenye hekima sasna machoni pao wenyewe na katika maamuzi yao yaliyopotoka. Kwa kupitia katika sera za wanadamu huwaongoza watu kufikiri kuwa amri za mungu zilizoelezwa dhahiri hazina nguvu kuliko desturi za wanadamu, na kufikiri kuw akupotosha sheria ambayo daima ni takatifu na ya haki na njema, ni jambo dogo tu. Anaona kwamba kwa kuwafanya wanadamu wasienende kama watoto watiifu kwa kupatana na Mungu, anaweza kuzuia kukamilika kwa kazi ya Mungu katika ulimwengu wetu.

Kadri mapambano yanavyosambaa katika maeneo mapya na mawazo ya watu kuelekezwa kwa sheria ya Mungu iliyokanyagwa chini, shetani anafadhaika. Nguvu inayoambatana na ujumbe huo itawatia wazimu wale wanaopinga. Viongozi wa makanisa watatumia juhudi zisizo za kawaida kuzuia isije ikawaangazia waumini wao. Kwa nji zozote zilizo katika uwezo wao watajaribu kukandamiza au kunyamazisha mijadala kuhusu maswali haya muhimu. Kanisa litaomba mkono wa nguvu wa serikali, na katika kazi hii Upapa na

Waprotestanti wanaungana. Kadri vuguvugu la kulazimisha Jumapili linavyozidi kuwa thabiti na dhahiri, sheria ya nguvu itatakiwa dhidi ya wale wanaozishika amri za Mungu. Watatishiwa kwa faini na kifungo, na baadhi watapewa nyadhifa kubwa, na wengine zawadi na upendeleo, kama kichocheo ili kukana imani.

[Shetani anasema:] "Hivyo ulimwengu utakuwa wangu. Nitakuwa mtawala wa dunia, mfalme wa ulimwengu. Nitatawala fikra za watu chini ya nguvu zangu ili kwamba sabato ya Mungu iwe jambo la kudhihakiwa. Ishara? Nitafanya utunzaji wa siku ya saba iwe ishara ya kutotii mamlaka za dunia. Sheria za wanadamu zitafanya kuwa ngumu sana ili kwamba wanaume na wanawake wasithubutu kuitunza sabato ya siku ya saba. Kwa hofu ya kukosa chakula na mavazi, wataungana na ulimwengu kuvunja sheria ya Mungu. Dunia yote itakuwa chini ya udhibiti wangu."

Lakini wakati dunia itakapoondoa sheria ya Mungu, matokeo yake yatakuwa nini kwa watii wa kweli na wenye haki? Je watachukuliwa na mkondo wenye nguvu wa uovu? Kwa sababu wengi sana watajiunga chini ya bendera ya mfalme wa giza, je, watu wa Mungu wanaozishika amri zake wataacha uaminifu wao? Kamwe! Hakuna hata mmoja akaaye ndani ya Kristo atakayeshindwa au kuanguka.

"Wakati umewadia Bwana atende kazi:
kwa kuwa wameitangua sheria
yako.

Ndiyo maana nimeyapanda maagizo yako.
Kuliko dhahabu, naana,
Dhahabu iliyo safi."

ZABURI 119:126,127

Wafuasi wake watasujudu kwa utii mamlaka iliyo kuu kuliko ya mtawala yeyote wa kidunia. Wakati dharau iliyopo juu ya amri za Mungu inawaongoza wengi kuukandamiza ukweli na kuonyesha heshima kidogo tu kwa huo, wale waaminifu kwa bdii sana watainua juu ukweli unaowatofautisha .

Wakati kinga ya sheria za kibinadamu itakapoondolewa kwa wale wanaoheshimu sheria ya Mungu, katika nchi mbali mbali kutakuwa na vuguvugu wakati uleule ili kuwaangamiza. Kadri muda uliowekwa kutekeleza hukumu hiyo utakavyokaribia, watu wataungana ili kuwafutilia mbali watu hao wanaochuiwa sana. Itakusudiwa kwamba washambuliwe usiku mmoja kwa pigo thabiti ambalo litanyamazisha kabisa sauti ya wale wasiokubali, na karipio.

Kwa makelele ya ushindi, dhihaka, na kulaani, makundi ya waovu yanakaribia tayari na kwa haraka ili kushambulia mateke wao, mara, loh, giza nene, zito kuliko giza la usiku juu ya nchi. Kisha upinde wa mvua, uking'aa kwa utukufu utokao kwenye kiti cha enzi cha Mungu, unaonenakana juu angani na unaonekana kuzingira kila kundi linaloomba. Umati wenye hasira ghafla unazuiwa. Kelele zao za kudhihaki zinatoweka. Lengo la hasira yao linasahauliwa. Kwa hisia ya utisho wa jambo baya linalotaka kutokea, wanatazama ishara ya agano la Mungu, na wanatamani kufichwa kutoka mwangaza wake wenye nguvu sana.

Kwa watu wa Mungu sauti inasikika, safi na yenye kupendeza, ikisema, "Tazama juu," na wanapoinua macho yao mbinguni, wanauona upinde wa ahadi, sauti inasikika tena yenye

kupendeza kama muziki na ya ushindi, ikisema: “Wanakuja! Wanakuja! Watakatifu, wasio na madhara, na wasiotiwa unajisi. Wamelishika neno la subira yangu; iliyopauka, yenye kutetemeka ya wale walioshikilia imani yao, inatamka kilio cha ushindi.

“Heri wazishikao amri zake, wawe
na haki ya kuuendea mti wa uzima,
na kuingia mjini kwa milango
yake.’

UFUNUO 22:14

Furaha Milele

Mbele ya waliokombolewa kuna mji mtakatifu. Yesu anayafungua malango ya lulu, na mataifa ambao wameutunza ukweli waningia ndani. Pale wanatazama paradiso ya Mungu, makao ya Adamu kabla ya dhambi. Ndipo ile sauti, tamu kuliko muziki wowote aliowahi kuusikia.” “Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu.

Waliokombolewa wanapokaribishwa mjini mwa Mungu, kinasikika hewani kilio cha shangwe cha kusifu. Adamu wawili wanakaribia kukutana. Mwana wa Mungu ana simama akiwa amenyoosha mikono yake ili kumlaki baba wa uzao wa wanadamu – kiumbe aliyemuumba aliyetenda dhambi dhidi ya muumba wake, na ambaye kwa dhambi zake alama za misumari ziko kwenye mwili wa mwokozi. Adamu anapotambua alama za misumari katili, haanguki kifuani pa Bwana wake, lakini kwa kujidhili anaanguka miguuni pake, akisema “amestahili, amestahili Mwana-kondoo aliyechinjwa!” kwa huruma mwokozi anamwinua juu na kumwambia aitazame tena Edeni, makao aliyokuwa amehamishwa siku nyingi.

Kwa furaha isiyosemeka anaona miti ambayo zamani ilimpendeza sana – miti ile hasa aliyokuwa amekusanya matunda yake katika siku zile za furaha na ambazo hakuwa na dhambi. Akili zake zinapokea uhalisi wa tukio; anatambua kuwa hakika hii ndiyo Edeni iliyorejeshwa, yenye kupendeza zaidi sasa kuliko wakati alipohamishwa, yenye kupendeza zaidi sasa kuliko wakati alipohamishwa, toka humo. Anatazama kando yake kuona umati wa famili yake uliokombolewa, ukiwa umesimama katika Paradiso ya Mungu. Ndipo wale waliozitunza amri za Mungu watapumua pumzi yenye nguvu ya kutokufa chini ya mti wa uzima; na katika miaka yote isiyo na mwisho wakazi wa malimwengu ambayo hayakuasi watatazama, katika ile bustani ya kupendeza, mfano wa kazi kamilifu ya uumbaji wa Mungu, ambayo hayakuasi watatazama, katika ile bustani ya kupendeza, mfano wa kazi kamilifu ya uumbaji wa Mungu, ambayo haikuguswa na laana ya dhambi – mfano wa jinsi ambavyo ulimwengu wote ungekuwa kama mwanadamu angetimiza mpango wa utukufu wa muumba wake.

Msalaba wa kristo utakuwa ni sayansi na wimbo wa waliokombolewa milele zote. Katika Kristo aliyetukuzwa watamwona Kristo aliyesulibiwa. Siri ya msalaba inatafsiri siri nyingine zote. Katika nuru inayotiririka kutoka Kalvari sifa za tabia ya Mungu ambazo zimekuwa zikitutia hofu na utisho zinaonekana nzuri na za kuvutia. Rehema, huruma, na upendo wa wazazi vinaonekana kuchangamana na utakatifu, haki na nguvu. Wakati tukiuona utukufu wa kiti chake cha enzi, juu na kilichoinuliwa sana, tunaiona tabia yake katika udhihirisho wa neema yake, na kufahamu, kupitia mwanzo, maana ya cheo kile cha kupendeza, “Baba Yetu.”

Mpango mkuu wa ukombozi unatokea kuuridisha tena ulimwengu chini ya upendo wa Mungu. Yote yaliyopotezwa kwa dhambi yanarejeshwa tena. Siyo tu mwanadamu lakini dunia imekombolewa, ili kuwa makao ya milele ya waaminifu. Kwa miaka elfu sita shetani ameshindana kudumisha kumiliki dunia. Sasa kusudi la Mungu la awali katika kuumbwa kwake linakamilika.

Sheria ya Mungu itasimama imara milele, na itakuwepo katika nchi mpya milele zote. Katika uumbaji, wakati misingi ya dunia ilipowekwa, wana wa Mungu waliangalia kwa shauku kazi ya Muumbaji, na majeshi yote ya mbinguni walishangilia kwa furaha. Ni wakati huo msingi wa sabato ulipowekwa. Mwishoni mwa siku sita za uumbaji, Mungu alistarehe siku ya saba akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya; akaibariki siku ya saba akaitakasa na kuitukuza. Sabato kamwe haitaondolewa; bali watakatifu waliokombolewa na majeshi yote ya malaika wataiadhimisha kwa heshima ya Muumbaji mkuu milele zote.

“Na itakuwa mwezi mpya hata mwezi mpya, na sabato hata sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA.” “Na kama vile mbingu mpya na nchi mpya, zitakavyofanya, zitakavyokaa mbele zangu, asema BWANA; ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa.” Isaya 66:23,22.

“Haki yako ni haki ya milele,
Na sheria yako ni kweli.”

ZABURI 119:142

Kamwe Sabato haitaondolowa; lakini watakatifu waliokombolewa na majeshi yote ya malaika wataiadhimisha kwa heshima ya Muumbaji mkuu milele zote.

Siku ya kupendeza

“Mtafanya kazi siku sita; lakini siku ya
saba ni sabato ya kustarehe kabisa, kusanyiko
takatifu; msifanye kazi ya namna yoyote; ni
sabato kwa BWANA katika makao yote.”

WALANI 23:3

UTAKATIFU WAKE

Mungu huwakaribia sana watu wake katika siku ile aliyoibariki na kuitaka. Kwa kufuata mfano wa muumbaji; mwanadamu alipaswa kupumzika katika siku hii takatifu, ili kwamba anapoziangalia mbingu na nchi, apate kutafakari kuhusu kazi kuu ya Mungu ya uumbaji; na kwamba anapoona ushahidi wa hekima na wema wa Mungu, moyo wake ujazwe na kicho na upendo kwa muumba wake.

JINSI YA KUANDAA

Katika muda wote tunapaswa kuwa na sabato akilini mwetu na kufanya matarisho ili kuitunza kwa kulingana na amri. Hatupaswi kuadhimisha tu sabato kama swala la kisheria.

Tunapaswa kuelewa umuhimu wake kirho katika shughuli zote za maisha. Kila siku litakuwa ombi la (watunza sabato) kwamba utakaso wa sabato uwe juu yao.

Wakati sabato inapokumbukuka hivyo, mambo ya kitambo tu hayataruhusiwa kuingiliwa mambo ya kiroho. Hakuna kazi ihusuyo siku sita itakayoachwa kufanyika siku ya sabato. Katikati ya wiki nguvu zetu hazitamalizwa kabisa na kazi za kawaida kiasi kwamba katika siku Bwana aliyopumzika na kustarehe tuwe tumechoka hata kushindwa kushiriki kwenye huduma yake.

Wakati matayarisho ya sabato yanapaswa kufanyika kwa wiki nzima, Ijumaa ni siku maalum ya maandalio. (Soma kutoka 16:23; Luka 23:50-56).

Katika (siku ya maandalio) tofauti zote kati ya ndugu, kwamba ni katika familia au kanissani, lazima ziondolewe.

Kabla sabato haijaanza, mawazo pamoja na miili pia vinapaswa kuondolewa katika shughuli za kidunia. Mungu anasema: “Wao wanaoniheshimu nitawaheshimu.” 1Samweli 2:30. Ni lazima kwa wivu tuilinde mipaka ya sabato. Kumbuka kwamba kila wakati ni wakfu na takatifu.

Kazi ambayo haikufanywa hadi sabato inapooanza inapaswa kuachwa hadi sabato imemalizika.

JINSI YA KUFUNGUA SIKU TAKATIFU YA MUNGU

“Nalifurahi waliponiambia, na twende nyumbani ka BWANA.” Zaburi 122:1.

“Haleluya, Nitamshukuru BWANA kwa moyo wangu wote, Barazani pa wanyofu wa moyo na katika mkutano.” Zaburi 111:1

“Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.”1Yohana 1:7.

Tunahitaji kudumisha na kukuza roho ya ibada ya kweli, roho ya kujitoa wakfu katika siku ya Bwana iliyo takatifu, iliyotakaswa. Tunapaswa kukusanyika pamoja tukiamini kwamba tutapata faraja na tumaini, nuru na amani kutoka kwa Yesu.

“kama ukigeuza mguu wako usiihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku bya furaha, na siku takatifu ya BWANA yenye heshima; ukiitukuza, kwakutozifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe, ndipo utkapojifurahisha katika BWANA; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha BWANA kimenena hayo.” Isaya 58:13,14.

Kila mmoja lazima ajisikie kwamba anayo sehemu ya kufanya ili mikutano ya siku ya sabato ipendeze. Haupaswi kukusanyika kama swala la desturi tu, lakini kwa ajili ya kubadilishana mawazo, kwa ajili ya uhusiano na uzoefu wa maisha ya kila siku ili kuonyesha shukrani, kwa ajili ya kutamka hitaji lako halisi la kuangaziwa nuru, ili upate kumjua Mungu, na Yesu

Kristo Aliyemtuma. Kushirikiana pamoja kumtafakari Kristo kutaimarisha roho kwa ajili ya majaribu na mapambano ya maisha.

Unapoingia mahali pa ibada, mwombe Bwana aondoe uovu wote moyoni mwako. Ingiza katika nyumba yake kile tu anachoweza kukibariki.

Pote nyumbani na kanisani roho ya huduma inapaswa kuonekana [siku ya sabato].

Mbingu zote zinaitunza sabato, lakini siyo kwa njia ya utepetevu na kutofanya lolote. Katika siku hiyo nguvu zote za roho zinapaswa kuamshwa, je, hatuendi kukutana na Mungu pamoja na Kristo Mwokozi wetu? Tunaweza kumwona kwa njia ya imani. Anatamani kuburudisha na kubariki kila roho.

Mahitaji muhimu ya maisha lazima yaangaliwe, wagonjwa lazima wahudumiwe, mahitaji ya wahitaji lazima yahudumiwe. Hatahesabiwa kuwa hana hatia yule asiyejali kupunguza mateso katika siku ya sabato. Siku ya Mungu ya kupumzika ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu, na hivyo matendo ya huruma yanakubaliana kwa ukamilifu na kusudi lake. Mungu hahitaji viumbe vyake kuteseka kwa maumivu hata ya saa moja yanayoweza kuponywa au kupunguzwa siku ya sabato au siku yoyote ile. Yesu alisema kwamba kazi yakuponya walioteseka ilikuwa inapatana na sheria ya sabato. (soma Luka 6:1-10).

“Basi ni halali kutenda mema siku ya sabato.” Mathew 12:12.

Shule ya sabato na ibada kuu huchukua sehemu tu ya sabato. Sehemu iliyobakia inaweza kufanywa kuwa wakati mtakatifu sana na wa thamani wa masaa yote ya sabato kwa familia. Sehemu kubwa ya muda huu wazazi waitumie pamoja na watoto wao. Katika hali nzuri ya hewa hemu wazazi watembee na watoto wao uwandani na penye miti mingi. Kati ya vitu vinavyopendeza vya asili waambie sababu ya kuwepo kwa sabato. Waambie kuhusu kazi kuu ya Mungu ya uumbaji. Waambie kwamba wakati dunia ilipotoka mikononi mwake, ilikuwa takatifu na nzuri ya kupendeza. Waonyeshe kwamba ni dhambi iliyoharibu kazi kamilifu ya Mungu. Waambie watazame jinsi dunia ambayo ingawa imeharibiwa na laana ya dhambi, bado inadhihirisha wema wa Mungu.

Waeleze habari za njia ya wokovu. Mweke Yesu mbele ya watoto, kama mtoto aliyewatii wazazi, kama kijana, alikuwa mwaminifu na mwenye bidii, akisaidia kutunza familia. Mara kwa mara soma pamoja nao visa ya kutuvutia vya Biblia. Waulize kile walichojifunza katika shule ya sabato, na usome pamoja nao somo la sabato inayofuata.

JINSI YA KUFUNGA MASAA MATAKATIFU YA SABATO

Jua linapoelekea kuzama, hebu sauti ya maombi na nyimbo za sifa zionyeshe kumalizika kwa masaa matakatifu na kumwalika Mungu katika masumbufu ya wiki ya kazi.

NENO KWA JUMAMOSI

Sabato

Kwa kweli lugha zote za ulimwengu, pamoja na zile za kale sana ambazo zimeendelea hadi leo, huthibitisha chimbuko la zamani za kale la wiki ya siku saba, ambalo huelezea siku ya saba kama sabato.

Majina ya siku ya saba ya wiki katika lugha mbalimbali

Lugha	Siku ya saba
Kiafghanista	Shamba
Kisiria Asili	Shabbatho
Kiarabu	Assabat
Kibabeli	Sabatu
Kibohemia	Sobota
Kibona (Afrika ya kati)	Sibta
Kibulgaria	Subbota
Kiethopia	Sanbat
Kifaransa	Samedi [Siku ya Sabato]
Kiyunani	Sabbaton
Kiebrania	Shabbath
Kihangari	Szombat
Kitalia	Sabbato
Kikurdi	Shamba
Kilatini	Sabbatum
Kilithuania	Subata
Maba [Afrika ya kati]	Sab
Kihimalaya	hari-Sabti [siku ya Sabato]
Kipoland	Sobota
Kireno	Sabbado
Kirumania	Sabat
Kirusi	Subbota
Kiswahili	Sabato
Kiserbia	Subota
Kihispania	Sabado
Kituruki	Yom-es-Sabt [Siku Sabato]
Kiurdu [India]	Shamba

Dazani za lugha zaidi kutoka Asia, Afrika, Ulaya na Mashariki ya Kati huonyesha siku ya saba kama “Sabato” katika lugha rahisi inayoeleweka.



KARNE YA KWANZA – AD (BK-Baada ya Kristo).

“ Kwa kuwa karibu makanisa yote ulimwenguni huadhimisha siri takatifu [Meza ya Bwana] katika sabato ya kila wiki.” Secrets Scholasticus, Eccl. History.

“Ndipo uzao wa kiroho wa Ibrahimu [Wakristo] wakakimbilia Pela, upande wa pili wa Yordani, walipopata mahali salama pa kukimbilia, na wangeweza kumtumikia Bwana wao na kuitunza Sabato yake.” Eusebius Ecclesiastical History.

Philo, mwanahistoria na falsafa, anathibitisha kwamba sabato hii ilikuwa katika siku ya saba ya juma.

KARNE YA PILI

“Wakristo wa zamani walikuwa na heshima kubwa kwa sabato, na walitumia siku hiyo katika ibada na mahubiri … inavyoonekana kwa maandiko kadhaa kwa kusudi hilo.” D.T.H. morer (church) of England) Dialogues on the Lords day, London, 1701.

KARNE ZA PILI, TATU, NNE

“Kutoka kwa mitume” hadi wakati wa Baraza la Laodikia (364 AD), adhimisho takatifu la Sabato ya Kiyahudi liliendelea, kama inavyoweza kuthibitishwa na waandishi wengi: naam, licha ya amri iliyotolewa dhidi yake.” John Ley, Jumapili ni sabato London, 1640.

KARNE YA TATU

Mwanzoni tu mnamo 225AD kulikuwa na dayosisi nyingi zilizokuwa zikitunza zikiwa ni za kanisa la Mashariki lililoenea tangu Palestina hadi India.” Mingana, Early Spread of Christianity.

KARNE YA NNE

“Katika kanisa la Milan (Italia) inaonekana kwamba Jumamosi ilichukuliwa kuwa ya heshima. Siyo kwamba kanisa la Mashariki au lolote katika yaliyobaki yaliyotunza siku hiyo, yalielekea dini ya Kiyahudi, lakini kwamba walikusanyika pamoja siku ya sabato kumwabudu Yesu aliye Bwana wa Sabato.” Dr. Peter Heylyn, History of the Sabbath, London, 1636.

“Kwa zaidi ya Karne 17 kanisa la Abyssinia liliendelea kuitakasa Jumamosi kama siku takatiu ya amri ya nne.” Ambrose de Morbius.

“Ambrose, askofu wa Milan aliyeadhimishwa, alisema kwamba alipokuwa Milan aliitukuza Jumamosi, lakini akiwa Rumi aliadhimisha Jumapili. Hili lilipelekea mithali inayosema “Unapokuwa Rumi, fanya kama Rumi inavyofanya” Heylyn, History of the Sabbath.

Uajemi 335-375 AD. “Wao [Wakristo] wanamdharau Mungu wetu jua. Je Zoroasta, mwanzilishi mtakatifu wa imani yetu ya miungu, hakuanzisha Jumapili miaka elfu moja iliyopita kwa heshima ya Jua na kutwaa mahali pa sabato ya Agano la kale? Na bado Wakristo hawa wana huduma takatifu siku za Jumamosi.” O’Leary, The Syriac Church Fathers.

KARNE YA TANO

“Augustine [ambaye ushahidi wake hufanywa wa kutuvutia sana kwa jinsi alivyo mtunza Jumapili aliyejitoa] anaonyesha … kwamba [siku ya saba] sabato iliadhimishwa katika siku zake, ‘katika sehemu kubwa ya ulimwengu wa Kikristo.”

Nicene and Post-Nicene Fathers. 1st Series, Vol.1, PP. 353, 354.

“Kuendelea hadi karne ya tano adhimisho la Sabato ya Kiyahudi liliendelea katika kanisa la Kikristo.” Lyman coleman, Ancient Christianity Exemplified. P. 526.

“Mnamo 411 [Mingana, kiongozi wa Makanisa ya Mashariki] alimteua mkurugenzi wa makao makuu kwa China. Makanisa haya yaliitakasa (Sabato) siku ya saba.” J.F. Colthor, The Sabbath Through the Centuries, P. 11.

KARNE YA SITA

“Katika mfano huu wa mwisho wao [Kanisa la Scotland] linaonekana uwa limefuata desturi ambayo tumepata alama zake katika kanisa la awali la kitawa la Ireland ambalo waliishika Jumamosi kuwa Sabato ambapo walipumzika kwa kazi zao zote.” W.T. skene, Adamnaris Life of St. Columba, 1874 P.96.

Kwa Kolumba wa Lona: “ Baada ya kufanya kazi katika Scotland kwa miaka thelathini na minne, kwa dhahiri na wazi alitabiri kifo chake, katika siku ya Jumamosi, tarehe tisa Juni, alimwambia mwanafunzi wake Diermit: “Hii ni siku inayoitwa Sabato, yaani, siku ya mapumziko, na hivyo ndivyo kweli itakavyokuwa kwangu; kwani itakuwa mwisho wa kazi zangu.” Butler’s Lives of the Saints, article on “st.Columba.’

KARNE YA SABA

“Inaonekana ilikuwa ni kawaida katika makanisa ya Celtic ya awali, katika Ireland kadhalika na Scotland, kutunza Jumamosi … kama siku ya mapumziko kwa kazi. Waliitii amri ya nne kwa vitendo katika siku saba ya juma.” Jas. C. Moffatt, The church in Scotland.

Kutoka Gregory 1, Papa wa Rumi 590-604: “Wenyeji wa Rumi: Nimepata habari kuwa watu fulani wenye roho tofauti wamepenyeza na kusambaza miongoni mambo ambayo ni maovu na yanayopingana na imani takatifu, kiasi kwamba wanakataza chochote kinachofanyika siku ya sabato. Niwaiteje watu hawa kama sio wahubiri wa mpinga-Kristo?”

KARNE YA NANE

India, China Uajemi, n.k. “Utunzaji wa sabato ya siku saba ulienea na kudumu miongoni mwa waumini wa kanisa la mashariki na Wakristo wa Mt. Thomas wa India, ambao kamwe hawakuungana na Rumi. Pia ilidumishwa miongoni mwa makundi yaliyojitenga na Rumi baada ya Baraza la Kalkedonia yakiitwa Waabisinia, Wayakobo, Wamarioni na Waarmenia.” New Schaff-Herroy Encyclopedia of Religious Knowledge, Article “Nestorians.”

“Katika siku ya saba tunatoa kafara, baada ya kusafisha mioyo yetu, na kupokea ondoleo la dhambi zetu. Dini hii, iliyo kamilifu na bora sasna, ni vigumu kutaja, lakini inaangaza gizani kwa kanuni zake zinazong’aa.”China 781 AD, The China Monument.

KARNE YA TISA

“Papa Nicholas I, katika karne ya tisa, alimtumia mfalme aliyetawala Bulgaria hati ndefu ikisema kuwa mtu anapaswa kutofanya kazi siku ya Jumapili, na siyo siku ya Sabato.

Kiongozi wa kanisa la kigiriki, akiwa amechukizwa na uingiliaji wa Papa, alitangaza kwamba Papa ametengwa na kanisa.” B.G. Wilkinson, Ph. D., Truth Triumphant p.232.

KARNE YA KUMI

“Wanestoria hawali nguruwe na wanatunza sabato. Hawaamini katika muungano ya faragha wala Purgatori.”New Schaff Herzog. Encyclopedia, Article, “Nestorians.”



KARNE YA KUMI NA MOJA

“Magret wa Scotland mnamo 1060 alijaribu kuangamiza wajukuu wa kiroho wa Kolumba kwa kutenda dhidi ya wale wote walioadhimisha sabato ya siku ya saba badala ya Jumapili.” Imeripotiwa na T.R. Barnett in Margaret of Scotland, Queen and Saint, P.97.

Yahusu kujitenga kwa kanisa la Kigiriki Kutoka kanisa la Kilatini mnamo 1054: “Utunzaji wa Jumamosi; kama kila mmoja anavyofahamu, ni swlal la mabishano makali kati ya – Wagiriki na Walatini.” J.M. Neale, A History of the Holy Eastern Church, vol 1.p.731.

KARNE YA KUMI NA MBILI

“Mabaki ya watunza-sabato yanapatikana katika … karne ya kumi na mbili huko Lombardy.” Strongs Encyclopedia.

Kwa Waldensia na 1120: “Utunzaji wa Sabato … umeamuriwa.” Blair, History of the Waldenses, vol. 1. P. 220.

Ufaransa: “Kwa miaka ishirini Peter de Bruys aliichochea ufaransa ya kusini. Hasa alisistiza siku ya ibada iliyokuwa ikitambuliwa kwa wakati huo miongoni mwa makanisa ya ki-celtic ya visiwa vya uingereza, miongoni mwa Wapaulisia, na katika kanisa kuu la Mashariki, iliyoitwa, siku ya saba ya amri ya nne.” Coltheart. P. 18.

KARNE YA KUMI NA TATU

“Sheria dhidi ya watunza-Sabato, Baraza la Toulouse, 1229: Sheria ya 3. Watawala wakuu wa wilaya mbalimbali watakuwa na makasri, nyumba, na misitu inayoangaliwa kwa bidii, na sehemu za maficho ya wazushi wanaoharibiwa. Sheria ya 4. Walei hawaruhusiwi kumiliki vitabu vya Agano la Kale au Jipya.” Hefele.

“Wapaulisiani, Wapetrobusiani, Wapasaginiani, Waldensia, Insabbatati yalikuwa makundi makubwa ya kutunza sabato katika Ulaya hadi 1250.” Coltheart, p. 19.

KARNE YA KUMI NA NNE

“Katika 1310, miaka mia mbili kabla ya maandishi ya Luther, ndugu wa Kibohemia walikuwa ni robo ya wakazi wa Bohemia, na waliwasiliana na Waldensia Walioishi Austria, Lombardy, Bohemia, Kaskazini ya Ujerumani, Thuringia, Brandenburg, na Morvia. Erasmus aliyonyesha wazi jinsi Waldensia wa Bohemia walivyotunza Sabato ya siku ya saba kwa makini kabisa.” Robert Cox, The Literature of the Sabbath Question, vol. 2, pp. 201, 202.

Norway: “Pia makasisi wamesababisha watu kutunza Jumamosi kama Jumapili.” Theological Periodicals for the Evangelical Church in Norway.” Vol.1, P.184.

KARNE YA KUMI NA TANO

“Erasmus anashuhudia kwamba hadi 1500 AD Wabohemia siyo tu kwamba waliitunza siku ya saba kwa wangalifu sana, lakini pia waliitwa Wasabatariani.” R. Cox. Op. Cit.

Norway, Baraza la Jimbo la Kikatoliki la Bergen, 1435: Tumearifiwa kwamba baadhi ya watu katika wilaya mbalimbali za Ufalme wetu, wamepokea na kuadhimisha utunzaji wa Sabato. Imeakatazwa kwa ukali kabisa - katika sheria za kanisa tkatifu – watu wote wadhimishe siku takatifu zile tu ambazo Papa mtakatifu, askofu mkuu, au maaskofu wameagiza. Utunzaji wa Jumamosi lazimakwa hali yoyo usiruhusiwe zaidi baada ya hapa, zaidi ya kanuni ya kanisa inavyoruhusu. Kwa hiyo tunawashauri wote wanaompenda Mungu nchini kote Norway wanaotaka kuwa watiifu kwa kanisa takatifu kuachana na uovu huu wa kutunza Jumamosi, na watakaobaki tutawakataza chin ya adhabu kali ya kanisa kwa kuitunza Jumamosi kuwa takatifu.” Dip. Norveg., 7,397.

KARNE YA KUMI NA SITA

Norway, 1544: “Baadhi yenu, kinyume na onyo lililotolewa, mnaitunza Jumamosi. Mnastahili kuadhibiwa vikali. Yeyote atakayepatikana akitunza Jumamosi lazima alipe faini ya Mark kumi.” Krag and Stephanius, History of King Christian III.

Liechtenstein: “Wasabatariani wanafundisha kwamba utunzaji wa nje wa sabato yaani Jumamosi, lazima uendelee kuadhimishwa. Wanasema kwamba Jumapili [kama siku ya ibada ya wiki] ni ubunifu wa Papa.” Wolfgang Capito, Refutation of the Sabbath, c.1590.

India: “Mjesuit maarufu, Francis Navier, aliomba uchunguzi, uliaoanzishwa kule Goa, India, mnamo 1560 ili kudhibiti “uovu wa Kiyahudi, yaani utunzaji wa Sabato.” Adeney, The Greek and Eastern Churches, pp. 527,528.

Abisinia: “Siyo kwa kuiga Wayahudi, lakini ni kwa kumtii Kristo na mitume wake watakatifu, kwamba tunaiadhimisha siku hiyo [Sabato].” From an Abyssinian Legate at the Court of Lisbon, 1534, quoted in Geddes’s Church History of Ethiopia, pp. 87,88.

KARNE YA KUMI NA SABA

“Karibu makanisa 100 yaliyotunza sabato, kwa uhuru, yalistawi nchini Uingereza katika karne ya 17 na 18.” Dr. Brian .W. Ball, The Seventh-Day Men, Sabbatarians and Sabbatarianism in England and Wales, 1600-1800, Clarendon Press, Oxford University, 1994.

[Kumbukumbu ya Mhariri: Sabato pia ilitunzwa katika sehemu mbalimbali za Ulaya na Amerika.]

KARNE YA KUMI NA NANE

Ujerumani: “Tennhardt wa Nuremberg anashikilia kwa nguvu kabisa fundisho la Sabato, kwa sababu ni mojawapo ya amri kumi.” J.A. Bengal, Leben und Wirken p.579.

“Kabla ya Zindendorf na Wamorvia katika Bethlemu [Pennsylavinia] hivi ukaanza utunzaji wa sabato na kufanikiwa, kulikuwa na kundi dogo la Wajerumani waliotunza sabato katika Pennsylvania.” Rupp, History of the Religious Denominations in the United States.

“Waabissinia na wengi wa bara la Ulaya, hassa Warumania, Wabohemia, Wamoravia, Uholanzi na Ujerumani waliendelea kuitunza Sabato. Popote kanisa la Rumi liliposhinda hawa watunza sabato waluvimilia kunyang’anywa mali zao, faini, kufungwa na kuaawa.” Coltheart, p. 26.

KARNE YA KUMI NA TISA

China: “Wataipei walipoulizwa kwa nini waliadhimisha sabato ya siku ya saba, walijibu, kwanza, kwa sababu Biblia ilifundisha, na pili, kwa sababu mababu zao waliiadhimisha kama siku ya ibada.” “A Critical History of Sabbath and Sunilay.”

“Kwa hiyo tunaona Dan. 7:25 ikitimizwa, pembe ndogo ikibadili “majira na sheria.” Hivyo ninaona kwamba wote waitunzao siku ya kwanza kama Sabato ni watunza – Jumapili wa Papa na wavunjai wa Sabato ya Mungu.” T.M. Preble, American Seventh Day Baptist, 1845.

KARNE YA ISHIRINI

[Kumbukumbu ya Mhariri: zaidi ya Wakristo milioni kumi wanaotunza Sabato ulimwenguni kati ya madhehebu zaidi ya 25 na mamia ya makundi yanayojitegema ya wale waitunzao sabato].

MAUNGAMO DHAHIRI

WAANGLIKANA

“Hakuna neno hata moja, wala dokezo, katika Agano Jipya linaloluhusu kutofanya kazi siku ya Jumapili … katika pumziko la Jumapili [yaani Jumapili kama siku ya mapumziko na ya ibada] hakuna sheria takatifu inayohusika… Adhimisho la Jumatano ya majivu au siku arobaini za kwaresma linasimama kwenye msingi ule ule wa adhimisho la Jumapili.” Canon eyton, the Ten Commandments.

“Ni wapi tunapoambiwa katika maandiko kwamba tuishike siku ya kwanza hata kidogo? Tumeamriwa kuishika siku ya saba; lakini hakuna popote tulipoamriwa kushika siku ya

kwanza … sababu inayofanya tuishike siku ya kwanza ya juma kuwa takatifu badala ya siku ya saba ni sababu ileile ambayo kwayo tunaadhimisha mambo mengine mengi, siyo kwa sababu Biblia imesema, bali kwa sababu kanisa limeamuru." Isaac Williams, D.D., Plain sermons on the Catechism, vol.1.pp. 334-336.

"Tumefanya mabadiliko kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza, kutoka Jumamosi kwenda Jumapili, kwa mamlaka ya kanisa takatifu la Katoliki." Bishop Seymour, Why we keep Sunday. Article 12.

WAKRISTO

"Hakuna mamlaka ya moja kwa moja ya Maandiko inayotaja siku ya kwanza kama siku ya Bwana." Dr. D.H. Lucas, Christian Oracle, Jan. 23, 1890.

"Siamini kwamba siku ya Bwana iliingia badala [mahali] ya sabato ya Kiyahudi, au kwamba sabato ilibadilishwa kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza, kwa sababu hii ya wazi, pale pasipo na ushahidi, hapawezi kuwa na imani. Sasa hakuna ushuhuda wowote katika unabii kwamba sabato ilibadilishwa, au kwamba siku ya Bwana ilichukua mahali pake." Alexander compbell, Washington Reporter, Oct. 8, 1821.

[Ukumbusho wa Mhariri: Basi kwa nini anaendelea kuiita Jumapili siku ya Bwana?]

WABAPTISTI

"Tunaamini kwamba sheria ya Mungu ni kanuni ya milele na isiyoharibika ya serikali yake ya Adili." Baptist Church Manual.

"Amri nne za kwanza huweka wazi wajibu wa mtu kuelekea kwa Mungu moja kwa moja… Amri ya nne huweka wazi madai ya Mungu katika muda na mawazo ya mtu … Hakuna neno [amri] hata moja kati ya zile kumi ambayo ina mipaka ya Utaifa fulani tu … Sabato ilianzishwa mwanzo [muda mrefu kabla ya Musa] pasipo uhusiano wowote na Waebrania, lakini kama desturi kwa wanadamu wote kwa ukumbusho wa pumziko la Mungu baada ya siku sita za uumbaji, ilikusudiwa kwa ajili ya uzao wote wa Adamu." Adult Quarterly, Southern Baptist Convention Series, Aug. 15, 1937.

"Kulikuwa na bado kuna sheria kuitakasa sabato, lakini siku hiyo ya sabato haikuwa Jumapili … Hata hivyo itasemwa, na kwa wengine ikiwa pamoja na onyesho la ushind, kwamba Sabato ilihamishwa kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza ya wiki … Ni wapi kumbukumbu za jambo kama hilo zinapoweza kupatikana? Siyo katika Agano jipya – sio kabisa. Hakuna ushahidi wa maandiko kwamba sabato ilibadilishwa kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza ya wiki.

"Kwangu mimi inaonekana ni jambo lisiloweza kuelezeka kwamba Yesu, katika kukutana na wanafunzi wake kwa miaka mitatu, mara kwa mara akizungumza nao kuhusu swala la Sabato … kamwe hakuzungumzia kubadilishwa kwa siku japo isiwe kwa wazi; na pia kwamba katika kipindi cha siku arobaini baada ya kufufuka, hakuna jambo kama hilo lililotangazwa.

"Naam, ninajua vizuri sana kwamba Jumapili ilianza kutumika katika historia ya awali ya Ukristo kama siku ya kidini, kama tunavyosoma kutoka kwa mababa na vyanzo vingine. Lakini ni jambo la kuhuzunisha jinsi gani inapokuja ikiwa ina alama ya upagani, na

kubatizwa kwajina la Mungu-jua, ilipotwaliwa na kuidhinishwa kwa uasi wa Papa, na kurithishwa kama dhamana kwa Uprotestanti!" Dr. Edward T. Hiscox, author of the Baptist manual (Still in Print), in a paper read before New York minister's conference held Nov. 13, 1893.

CONGREGATIONALIST:

"Ni lazima ikubalike kwamba hakuna sheria yoyote katika Agano Jipya kuhushu siku ya kwanza." Bucks Theological Dictionary.

"Mawazo ya karibuni kwamba Kristo na mitume wakekwa mamlaka waliweka siku ya kwanza badala ya siku ya saba, halina kabisa mamlaka katika Agano Jipya." Dr. Lyman Abbott, Christian Union, Jan. 19, 1882.

WALUTHERI

"Ninashangaa sana jinsi ilivyopandikizwa kwangu hata niikatae sheria ya amri kumi … Yeyote atakayeondoa sheria lazima aondoe dhambi pia." Martin Luther, Spiritual Anti Christ, pp. 71, 72.

"Wao [Wakatoliki] wanadai kuwa sabato ilibadilishwa kwenda Jumapili, siku ya Bwana, kinyume na amri kumi, kama inavyooneka, wala hapana mfano wowote wanaojivunia zaidi kuliko kubadilisha Sabato. Wanasema uwezo wao ni mkuu na mamlaka ya kanisa, kwa kuwa liliondoa moja ya amri kumi." Martin Luther, Angsburg Confession of Faith, Art. 28, Par. 9.

Lakini wanakosea katika kufundisha kwamba Jumapili imeachukua mahali pa Sabato ya Agano la kale na hivyo lazima itunzwe kama siku ya saba ilivyotunzwa na wana wa Israeli. Kwa maneno mengine, wanasisitiza kwamba Jumapili imewekwa na Mungu kama Sabato ya Agano Jipya, na hivyo wanajaribu kulazimisha utunzaji wa Jumapili kama sabato kwakile kinachoitwa sheria za bluu … Makanisa haya yanakosea katika mafundisho yao, kwa kuwa Maandiko hayajaagiza kwa namna yoyote siku ya kwanza ya Juma kuwa badala ya Sabato. Kwa kifupi hakuna sheria katika Agano Jipya kwa matokeo hayo." John T. Mueller, Sabbath or Sunday?, pp 15, 16.

WAMETHODISTI

"Haya 'maandishi ya mkono ya amri' Bwana wetu aliyaondoa, aliyafuta, na kuyagongomelea kwenye msalaba wake. (Wakolosai 2:14). Lakini sheria ya maadili iliyomo katika amri kumi, na kutiliwa mkazo na manabii, hakuiondoa … sheria ya maadili inasimama katika msingi tofauti kabisa na sheria za sikukuu au taratibu zake … Kila sehemu ya sheria hii lazima ibakie na nguvu kwa watu wote na katika vizazi vote." John Wesley, Sermons on Several Occasions, 2 vol. ed., vol. 1, pp 221, 222.

"Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu; siyo kwa Waebrania, bali kwa watu wote." E.O. Haven, Pillars of Truth, p.88.

"Watu walikuwa Wakristo na walitawaliwa na mfalme aliyeitwa Constantino [312-327 AD]. Mfalme huyu aliifanya Jumapili kuwa Sabato ya Wakristo, kwa sababu ya mibaraka ya mwanga na joto vilivyotoka kwenye jua. Hivyo Jumapili yetu ni siku ya jua, au siyo?" Sunday School Advocate, Dec. 31, 1921.

[Uk. Mhariri: Thiologia ya ndani jinsi gani!].

TAASISI YA MOODY YA BIBLIA

“Sabato ilikuwa shurti katika Edeni, na imekuwa wajibu tangu hapo, Amri ya nne inaanza na neno “Ikumbuke” ikionyesha kwamba Sabato tayari ilikuwepo wakati Bwana alipoandika sheria katika mbao za mawe pale Sinai. Watu wanawezaje kudai kwamba amri hii moja imeondolewa wakati wakikiri kwamba zile nyingine tisa bado zinawafunga?” Dwight L. Moody, Weighed and Wanting, p. 47.

“Wakati Kristo alipokuwa duniani hakufanya chochote kuiweka [Sabato] kando; aliiweka huru kutoka chembechembe ambazo waandishi na Mafarisayo waliziingiza, na kuiweka ilipostahili. ‘Sabato ilifanyika kwa ajili ya Mwanadamu, na sio mwandamu kwa ajili ya Sabato.’ Ni jambo la kuweza kufanyika na la muhimu kwa watu leo kama lilivyokuwa siku zote – kwa kweli, zaidi ya siku zote, kwani tunaishi katika kipindi cha hisia kali.” Ibid., p.46.

Sabato ilikuwa wajibu
Katika Edeni, na imekuwa ni
Wajibu tangu hapo.

PRESBYTERIAN:

“Sabato ni sehemu ya amri kumi. Hili pekee humaliza au kujibu swali kuhusu umilele wa desturi hii … Hadi hapo itakapoweza kuonyeshwa kwamba sheria yote ya maadili imetanguliwa, Sabato itadumu … Fundisho la Kristo huthibitisha umilele wa Sabato.” T.C. Blake, D.D., Theology Condensed, pp. 474, 475.

“Hatupaswi kufikiri kwamba kuja kwa Kristo kumetuweka huru na mamlaka ya sheria, kwani ni kanuni ya milele ya maisha matakatifu ya kujitoa, na hivyo lazima isiwe yenye kubadilika, kama ilivyo haki ya Mungu, inayoungamanishwa, ni ya daima na inafanana.” John Calvin, Commentary on a Harmony of the Gospels, vol.1, p.277.

“Kuhusu kudumu kwa sabato, tunaweza kutoa hoja kwa nafasi yake katika amri kumi, inaposimama ikitunzwa kati ya maadili ya wema yasiyobadilika na ya milele.” Thomas Chalmers, DD., Sermons, vol.1. p.51.

KUSEMA WAZI

S. Je kuna sehemu yoyote Maandiko yanapoagiza kushika Jumapili badala ya Sabato?

J. “Maandiko yanatuamuru kulisikia kanisa, Math. 18:17; Luka 10:16, na kushikilia mapokeo ya mitume, 2Wathes. 2:15, lakini hasa maandiko hayataji badiliko hili la sabato. Mt. Yohana anazungumzia siku ya Bwana, Uf. 1:10, lakini hatwambii ni siku gani ya wiki ilikuwa siku hiyo ingechukua nafasi ya Sabato iliyoamriwa katika amri kumi: Mt. Luka naye huzungumzia wanafunzi kukusanyika kuumega mkate siku ya kwanza ya Juma, Matendo 20:7, na Mt. Paulo, 1 Wakor. 16:2, anaagiza kwamba katika siku ya kwanza ya wiki Wakorintho wajiwekea akiba kile walichokusudia kutoa kwa uakrimu kwa waaminifu

walioko Uyahudi: lakini hakuna hata mmoja kati yao anayesema tangu hapo siku hiyo ya kwanza sasa ingekuwa siku ya ibada, na sabato ya Wakristo: kwa hiyo ukweli mamlaka bora tuliyo nayo kwa jambo hili ni ushuhuda na amri ya kanisa." Bishop Richard Challoner, "The Catholic Christian Instructed." 1737.

"Kutoka kwenye kanisa hili hili la Katoliki mmeipokea Jumapili yenu, na hiyo Jumapili, kama siku ya Bwana, limeendelea kukabidhi kama mapokeo; na ulimwengu wote wa Kiprotenstanti umeikubali kama mapokeo, kwani hamna hata nukta moja ya Maandiko kwa ajili ya kuianzisha. Kwa hiyo kile ambacho mmekikubali kama kanuni ya imani yenu, kwa jinsi ilivyo na upungufu, kama ilivyo Jumapili yenu, mmeikubali mamlaka ya Kanisa Katoliki la Rumi." D. B. Ray, The Papal Controersy, 1892, p.179.

"Nimerudia rudia kutoa dola 1,000 kwa yeyote anayeweza kunithibitishia kutoka katika Biblia tu kwamba ninafungwa kuitunza Jumapili kuwa takatifu. Hakuna sheria kama hiyo katika Biblia. Ni sheria ya kanisa takatifu Katoliki tu. Biblia inasema, 'ikumbuke siku ya Sabato uitakase.' Kanisa Katoliki linasema 'Hapana. Kwa uwezo wangu mtakatifu ninaondoa siku ya sabato na nawaamuru kuishika siku ya kwanza ya juma kuwa takatifu.' Na loh! Ulimwengu wote uliostaarabika unainama na kuheshimu kwa utii wa amri ya kanisa takatifu Katoliki." T. Enright, CSSR, in a lecture at Harford, Kansas, Feb. 18, 1884

"Kanisa Katoliki kwa zaidi ya miaka elfu moja kabla ya kuwepo Uprotenstanti, kwa sababu ya utume wake mtakatifu, lilibadili siku kutoka Jumamosi kwenda Jumapili … Sabato ya Wakristo [Jumapili] kwa hiyo imeafikiwa hadi leo kuw ani uzao wa kanisa Katoliki … bila neno la kupinga kutoka ulimwengu wa Kiprotestanti." The Catholic Mirror, Sept. 23, 1893.

"Unaweza kusoma Biblia tangu Mwanzo hadi Ufunuo, na hutapata mstari hata mmoja unaohalalisha kutakaswa kwa Jumapili. Maandiko yanatilia nguvu utunzaji wa kidini wa Jumamosi, siku ambayo sisi [Wakatoliki] kamwe hatuitakasi." James Cardinal Gibbons, The faith of Our Fathers, p. 111.

Thomaston, Georgia
May 22, 1934
Papa Pius XI
Roma, Italia

Bwana Mpendwa,
Ni ya kweli mashtaka ambayo Waprotestanti wanawashtaki?
Wanasema mlibadili Sabato ya siku ya saba kwa kile
Kinachoitwa Jumapili ya Wakristo: iliyo siku ya kwanza ya juma.
Kama ndivyo, na lini badiliko hilo lilifanyika na kwa mamlaka gani?
Wako mtiifu, J.L. Day.

"Busara na ufahamu unadai kupokelewa kwa moja au nyingine ya pande hizi mbili: Uprotestanti na utunzaji wa Jumamosi au Ukatoliki na utunzaji wa Jumapili kuwa takatifu. Kuridhia hakuwezekani." James Cardinal Gibbons, Catholic Mirror, Dec. 23, 1893.

“Hakuna popote katika Biblia tunaposoma kwamba Kristo au mitume waliagiza kwamba Sabato ibadilishwe kutoka Jimamosi kwenda Jumapili. Tunayo amri ya Mungu alyopewa Musa ya kuitakasa siku ya Sabato, hiyo ni siku ya saba ya Juma. Jumamosi. Leo Wakristo wengi wanashika Jumapili kwa sababu imefunuliwa kwetu na Kanisa [Katoliki] nje ya Biblia.” Catholic Virginia, Oct. 3, 1947.

Jumapili ni desturi ya Kikatoliki, na madai yake ya kuadhimisha yanaweza tu kutetewa kwa kanuni za Kikatoliki … Toka mwanzo hadi mwisho wa maandiko hakuna hata aya moja inayoidhinisha uhamisho wa siku ya ibada ya jamii ya wiki kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza.” Catholic Press, Sydney, Australia, August 25, 1900.

“Jumapili haikujengwa, katika Maandiko, bali katika mapokeo, na kwa utambulisho ni desturi ya Kikatoliki. Kwa vile hakuna andiko kwa mabadiliko ya siku ya mapumziko kutoka ya mwisho kwenda siku ya kwanza ya juma, Waprotestanti wanapaswa kushika sabato yao siku ya Jumamosi na hivyo kuwaachia Wakatoliki umiliki kamili wa Jumapili.” Catholic Record, September 17, 1893.

“Dayosisi ya askofu mkuu wa Baltmore inathibitisha: “Mwe na hakika, rafiki zenu Waadventista Wasabato wanawaambia ukweli, wanaposema kwamba ni kanisa la Katoliki lililobadili siku ya kuabudu kutoka sabato ya Wayahudi hadi Jumapili ya Wakristo … ikiwa Uprotestanti utafuata Biblia, watamwabudu Mungu katika siku ya Sabato. Kwa kuitunza Jumapili wanafuata sheria ya kanisa Katoliki. Wakati wa karne tatu za kwanza mazoea na mapokeo yaliweka wakfu Jumapili kwa ajili ya kumwabudu Mungu.” Letter to Mrs. Ashby, February 10, 1920.

Bertrand Conway anasema: “Kama Biblia mwongozo pekee kwa Wakristo, basi Waadventista Wasabato wako sahihi kwa kuishika sabato na Wayahudi. Lakini Wakatoliki wanajifunza ni nini waamini na kutenda kutoka kwa mamlaka matakatifu, yasiyokosea … ya kanisa Katoliki.” Question Box, p. 179.

Father Walter Drum anasema: “Wao [Waprotestanti] wana maoni kwamba ni wajibu wao kuitunza Jumapili kuwa takatifu. Kwa nini? Kwa sababu kanisa Katoliki linawaambia kufanya hivyo. Hawana sababu nyingine … Hivyo adhimisho la Jumapili linakuwa ni sheria ya kichungaji ambayo ni tofauti kabisa na sheria takatifu ya utunzaji wa Sabato … Mwanzilishi wa amri ya Jumapili … ni Kanisa Katoliki.” Ecclesiastical Review, February, 1994.

Ifuatayo ni barua ya kujibu barua ya J. L. Day aliyeuliza kwenye barua iliyotanguka

THE CATHOLIC EXTENSION MAGAZINE
180 Wabash Ave., Chicago, Illinois
(Kwa baraka za Papa Pius XI)

Mpendwa bwana:

Kuhusu badiliko kutoka kwenye utunzaji wa sabato ya Kiyahudi kwenda Jumapili ya Wakristo, ninapenda kuelekeza mawazo yako kwenye kweli zifuatazo.

(1) Kwamba Waprotestanti, wanaoikubali Biblia kama kanuni pekee ya imani na dini, lazima kwa njia zote warejee katika utunzaji wa Sabato. Ukweli kwamba hawafanyi hivyo, lakini kinyume chake wanaadhimisha Jumapili, hufanya waonekane wapumbavu machoni pa kila mtu mwenye kufikiri.

(2) Sisi Wakatoliki hatuikubali Biblia kama kanuni pekee ya imani. Licha ya Biblia tunalo kanisa lililo hai, mamlaka ya kanisa, kama kanuni ya kutuongoza. Tunasema kanisa hili, lililoanzishwa na Kristo kufundisha na kuwangoza watu maishani, lina haki ya kubadili sheria za sikukuu za Agano lakale; na hivyo, tunakubali mabadiliko ya Sabato kwenda Jumapili. Kwa wazi, tunasoma "Ndiyo, kanisa lilifanya mabadiliko, liliweka sheria hii, kama lilivyofanya kwa kuweka sheria nyingine nyingi, kwa mfano kufunga siku zas Ijumaa, ukasisi wa wasiooa sheria kuhusu ndoa mchanganyiko, taratibu za ndoa za Kikatoliki, na maelfu mengine ya sheria.

(3) Pia tunasema kwamba kati ya Waprotenstanti wote, Waadventista Wasabato ndilo kundi pekee linalofikiri sawasawa na wanakubaliana na mafundisho yao. Mara zote inachekesha kiasi kuona makanisa ya Kiprotestanti, mimbarani na mabarazani, wakidai kuadhimishwa kwa Jumapili, ambako hakuna agizo la Biblia.

Kila la Kheri,

Peter R. Tramer, Editor (imesainiwa)

[Kumb. ya Mhariri: Kwa nguvu ya maelezo haya dhahiri na utafiti wake wa kujifunza Biblia, Mr. Day aliamua kuwa Mwadventista Msabato.]

BIBLIA INASEMA …

1. Ni lini Sabato ilifanyika?

"Basi mbingu na nchi zikamalizika na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya." Mwanzo 2:1-3. Mungu alianzisha Sabato (sambasamba na ndoa) katika siku ya mwisho ya wiki ya uumbaj, wakati dunia ilipokuwa katika ukamiifu wake wa mwanzo (Mwanzo 1:3) kabla mtu hajatenda dhambi na kabla hajaumba mataifa. Kwa hiyo sabato ilitolewa kwa wanadamu wote na siyo sehemu tu. Elimu ya asili na kukua kwa maneno inaonyesha kwamba kwa Kiebrania-Sabato humaanisha ""shara ya Baba Muumbaji."

2. Nani alifanya Sabato?

"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" Hapo mwazo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chocho kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu … Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu (nasi tukauona utukufu wake, utukuf kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba), amejaa neema na kweli." "Mungu,

aliyeviumba vitu vyote katika Yesu Kristo." Mwanzo 1:1; Yohana 1:1-4,14; Waefeso 3:9; Math. 12:8.

3. Sabato ilifanyika kwa ajili ya nani?

   "Naye kasema [Yesu] … Sabato ilifanyika kwa ajili ya Mwanadamu, Si mwanadamu kwa ajili ya Sabato." Marko 2:27. Mungu hakumwumba mtu kutunza siku, bali siku ili mwanadamu aitunze. Ikiwa imetolewa kwa makusudi matakatifu, zawadi yake ya masaa matakatifu haipaswi kuhafifishwa, kufanyiwa dhihaka, au kutojaliwa.

4. Ni hadhi gan maalum aliyoipatia sabato na ni kwa nini? Mungu aliijumuisha sabato kama amri ya nne kati ya amri kumi zilizoandikwa kwa chanda chake kwenye mbao za mawe: "I"umbuke siku ya sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utnde mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifsanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa." "Amefanya ukumbusho wa matendo yake ya ajabu; BWANA ni mwenye Matendo ya mikono yake ni kweli na hukumu, maagizo yake yote ni amini, Yamethibitika milele na milele." Kutoka 20:8-11; Zaburi 111:4-8. Ni ukumbusho wa viumbe vyake na uumbaji wake. Kwa kuwa Mungu aliwaumba wanadamu wote, sabato inauhusu ulimwengu wote.

5. Ni kwa miujiza gani uliofanyika kabla ya sinai ambao kwa huo Muumbaji aliitofautisha na Kuithibitisha sabato kama siku ya utakatifu wa mibaraka maalum? "Ndipo BWANA akamwambia Musa, Tazama, mimi nitawanyeshea ninyi mvua ya mkate kutoka mbinguni; na hao watu watatoka nje na kuokota kila siku sehemu ya siku; ili nipate kuwajaribu, kwamba watakwenda katika sheria yangu, ama sivyo, kisha itakuwa siku ya sita, ya kwamba watyaandaa hayo watakayoleta ndani, nayo yatakuwa ni mara mbili kuliko wayaokotyo kila siku."Kutoka 16:4,5, soma pia fungu la 14-30. Mungu alirudia muujiza wa mana na sehemu yake maradufu kwa ajili ya Sabato kila wiki kwa muda wa miaka 40, hivyo kuithibitisha kabisa Sabato mara 2,080 na kuonyesha umuhimu wa siku hiyo mbele zake.

6. Ni nani Bwana wa Sabato, naye anaiitaje siku hiyo? "Kwa maana Mwana wa Adamu ndye Bwana wa Sabato" Math. 12:8. "Nilikuwa katika Roho siku ya Bwana." Uf. 1:10.

7. Ni ahadi gani anazoziongeza kwa wale wanaoitunza sabato yake takatifu? "Kama akigeuza mguu wako usiihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya BWANA yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika BWANA; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha BWANA kimenena hayo." Isaya 58:13,14.

8. Zaidi ya kukumbusha uumbaji wake sabato, ni kazi gani nyingine Mungu ameipa siku yake takatifu?

   "Tena naliwapa Sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao, wapate kujua ya kuwa mimi, BWANA, ndimi niwatakasaye … zitakaseni Sabato zangu; nazo zitakuwa ishara

kati ya mimi na ninyi, mpate kujua ya kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wenu." Ezekieli 20:12,20. Kama ishara ya uwezo wake kutakasa watu wake, sabato hutenda kama muhuri (soma Warum 4:11) wa agano lake alilofanya na wale wanaomwabudu kuingana na maagizo yake. Inahitaji uwezo wa uumbaji mpya kuokoa na kutakasa mwanadamu aliyeanguka. Kwa hiyo sabato ukifikiri vizuri ina kazi mbili, ya kumtukuza Mungu kama Muumbaji na mkombozi wetu (yaani anyeumba upya, soma Zaburi 51:10-12; Waefeso 4:23,24).

9. Je Kristo alishika au kutunza Sabato?

   "Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome." Luka 4:16. "Yesu akasema, mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake." Yohana 15:10. Ni wazi, Yesu alikuwa mtunza Sabato, aliyetii amri kumi, pamoja na ya nne, ambayo ni ya sabato. Kristo alieleza kwamba utii wa Amri ni tundala upendo wa Mungu, siyo matokeo ya desturi, ushupavu wa sheria au upofu kwa Injili (Soma Math. 5:17-20; Yohana 14:15; 15:9-11; Waebr. 13:8) Amri ya kumpenda Mungu kuliko vyote na jirani kama nafsi yako haichukui nafasi ya Amri kumi, bali huelezea au kufafanua umuhimu wake (soma Math. 22:36-40; Walawi 19:18; Kumbukumbu 6:5) Yesu hakuvunja Sabato, kama wengine wanavyodai, lakini aliiondolea desturi zisizo za Kibiblia ambazo waalimu wa kidini walizibuni chini ya uvuvio wa Shetani. Soma Math. 12:1-15, (15:6-9); Luka 13:10-17; Marko 7;9-13. Kwa dhahiri, Yesu alionyesha kwamba Sabato ya Biblia itaendelea hata baada ya kusulibiwa na kufufuka kwake, bila kugusia kwamba itakomeshwa au kubadilishwa. (Soma Math. 24:20,21; Luka 16:17) Wakristo wanapaswa kufuata mfano wa Kristo, unaohusisha utunzaji wa sabato ya siku ya saba. (1Yoh. 2:5,6; Yoh. 13:15-17; 1Petro 2:21)

10. Kristo alithibitishaje sabato baaa ya kifo chake? "Mtu huyo … akataka kupewa mwili wa Yesu. Akaushusha … akauweka katika kaburi … Na siku ile ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia." Luka 23:52-54. Baba na Mwana walipumzika siku ya Sabato baada ya kazi yao ya kwanza kubwa, kazi ya Uumbaji. Sasa Yesu, baada y akumaliza kazi yake ya pili kuwa – kazi ya ukombozi, anapumzika tena katika siku ya Sabato kabla ya kufufuka kwa utukufu wa ushindi.

11. Je, wanafunzi walitunza sabato baada ya Yesu kusulibiwa? "Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na siku ya sabto walistarehe kama ilivyoamriwa." "Na walipokuwa wakitoka, wakawasihi waambiwe maneno haya Sabato ya pili … Paulo na Barnaba … wakisema nao, wakawatia moyo kudumu katika neema ya Mungu. Hata sabato ya pili, watu wengi, karibu mji wote, wakakusanyika walisikie neno la Mungu."'Hata siku ya sabato tukatoka nje ya lango, tukaenda kando ya mto, ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali; tukaketi, tukasema na wanawake waliokutna pale." "Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko Sabato tatu." "akatoa hoja zake katika Sinagogi kila Sabato tatu." "Akatoa hoja zake katika Sinagogi kila Sabato, akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani." (Luka 23:56; Matendo 13:42-44; 16:13; 17:2; 18:4).

12. Ni kwa jinsi gani na kwa nini Mungu anasisitiza haja ya kutunza Sabato katika siku hizi za mwisho, kabla ya marejeo ya Yesu?

Jinsi gani: “Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa, na kabila, na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemichemi za maji.” Uf. 14:6,7. (Linganisha na Kutoka 20:11; Soma pia Uf. 14:12; 22:14.

Kwa nini: “Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa… kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako.” “Nijapomwandikia sheria yangu katika amri elfu kumi, zimehesabiwa kuwa ni kitu kigeni: Maana Israeli amemsahau Muumba wake.” “Umevidharau vitu vyangu vitakatifu, umezitia unajisi sabato zangu … Makuhani wake wameihalifu sheria yangu … nao wamefumba macho yao, wasiziangalie sabato zangu.” Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu.” Hosea 4:6, 8:12,14. Ezekieli 22:8,26; Uf. 12:17. (Soma pia Isaya 56:1-8)

13. Ni kwa upekee gani maalum Sabato ya Siku ya saba inakuwa muhuri wa Mungu? (Soma tena kut. 20:8-11, Kumbukumbu 4:13; Waebrania 8:10-12; Ezek. 20:12,20; Kut. 31:13-18. Soma pia Isaya 56:1-8; Maombolezo 1:7; Ezek. 22:8, 26; Neh. 13:15-18; Zab. 119:126, 127)

    a) Mungu kwa dhahiri huielezea kama ishara ya agano na watu wake.
    b) Katika amri zote kumi ni Sabato pekee iliyo na muhuri rasmi wa mtoa sheria; Jina lake (Bwana Mungu, wako); cheo (Muumbaji – Yeye aliyeufanya ulimwengu); Eneo analotawala (Ulimwengu wote, na viumbe vyake).
    c) Anaonyesha wazi kwamba Sabato itadhihakiwa na kudharauliwa na wapagani na waasi wanaodharau mamlaka yake ya Uumbaji. Kwa hiyo Mungu anaitukuza Sabato kuwa na hadhi ya kuheshimiwa; na hasa kwa sababu watu wake watateswa kwa sababu ya kuitunza badala ya Jumapili, ambayo ni Sabato bandia.

15. Ni alama gani maalum wanayopata wale wanaokataa kumwabudu Muumbaji, badala ya muhuri wake mkuu, Sabato?

    “Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-kondoo, akanena kama joka … Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.”

    “Ndiyo kanisa Katoliki linadai kwamba badiliko [toka Sabato kwenda Jumapili] ni tendo lake. Na tendo hilo ni ALAMA ya uwezo wake wa kikasisi na mamlaka katika mambo ya kidini.” C.F. Thomas, Chancellor of Cardinal Gibbons of Baltimore.

    “Busara na ufahamu hudai kupokelewa mojawapo ya pande hizi mbili: Uprotestanti na kuitunza Jumamosi kuwa takatifu au Ukatoliki na kuitunza Jumapili. Maridhiano ni jambo lisilowezekana.” James Cardinal Gibbons, Catholic Mirror, Dec. 23, 1893.

16. Nini wito maalum wa Mungu kwa watu wote?

"Mcheni Mungu na kumtukuza." "Chagueni hivi leo mtakayemtumikia." "Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu." "Laiti ungalisikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari." "Heri wazishikao amri zake, wawe na amri ya kuuendea mti wa uzima, na kuingia mjini kwamilango yake." Uf. 14:7; Yoshua 24:15; Matendo 5:29; Isaya 48:16-18; Ufunuo 22:14.

SHERIA YA MUNGU

AGANO LA KALE	AGANO JIPYA	KAMA ILIYOBADILISHWA NA MWANDAMU
I Usiwe na Miungu mingine ila Mimi.	I "Msijudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake." Math. 4:10	I Mimi ni Bwana Mungu wako. Usiwe na miungu migeni mbele zangu. [Utagundua ya kuwa amri ya pili kama ilivyo katika Biblia imeachwa nje.]
II Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia. Kwa kuwa Mimi, BWANA, Mungu wako ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao na kuzishika amri zangu	II "Watoto wadogo, jilindeni nafsi zenu na sanamu" "Basi, kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu, haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili za wanadamu." 1 Yohana 5:21; Matendo 17:29	II Usilitaje burejina la Bwana Mungu wako.
III Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure	III "Jina la Mungu lisitukanwwe wala mafundisho yetu." 1 Timotheo 6:1	III Kumbuka kushika kitakatifu siku ya Sabato [au siku ya Bwana]. [Katekisimu ya mafundisho," (Katoliki) uk. 174 ina swali na jibu lifuatalo: "S- Je, mnayo njia nyingine yoyote ya kuthibitisha kuwa kanisa lina uwezo wa kuanzisha kanuni za sikukuu?" "J- Kama lisingekuwa na uwezo huo … lisingewezsa kuweka adhimisho la Jumapili, siku ya kwanza ya juma, badala ya Jumamosi, siku ya saba, badiliko ambalo halina mamlaka ya Maandiko."]
AGANO LA KALE	**AGANO JIPYA**	**KAMA ILIYOBADILISHWA**

		NA MWANDAMU
IV Ikumbuke siku ya Sabato uitakase, siku sita fanya kazi	IV “Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wabaridi wala siku ya Sabato.” “Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwadamu, si mwandamu kwa ajili ya Sabato: Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato pia.” “Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi, Mungu alistarehe siku ya saba, akaziacha kazi zake zote.” “Basi imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake.” “Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi.” Mathayo 24:20; Marko 2:27,28; Waebrania 4:4,9,10; Wakolosai 1:16.	IV Waheshimu baba yako na mama yako.
V Waheshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako	V “Waheshimu baba yako na mama yako”Mathayo 19:19	V Usiue
VI Usiue	VI “Usiue.” Warumi 13:9	VI Usizini
VII Usizini	VII “Usizini.” Mathayo 19:18	VII Usiibe
VIII Usiibe	VIII “Usiibe.”Warumi 13:9	VIII Usimshuhudie jirani yako uongo.

AGANO LA KALE	AGANO JIPYA	KAMA ILIYOBADILISHWA NA MWANDAMU
IX Usimshuhudie jirani yako uongo.	IX "Usishuhudie Uongo" Warumi 13:9	IX Usimtamani mke wa jirani yako.
X Usitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala chochote alichonacho jirani yako. SOMA Kutoka 20:1-17 "MIMI SITALIHALIFU AGANO LANGU, SITALIBADILI NENO LILILOTOKA MIDOMONI MWANGU." Zaburi 89:34	X "Usitamani" Warumi 7:7 Baada ya kifo chake "Basi, je! twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume chake twaithibitisha sheria." Warumi 3:31 "Wakastarehe siku ya Sabato kama ilivyoamriwa" Luka 23:54-56	X Ustamani mali ya jirani yako. [Angalia-Katekisimu kuu ya Kikatoliki.] "ATAAZIMU KUBADILI MAJIRA NA SHERIA." Daniel 7:25 "…Mtu wa kuasi…yule mpingamizi, ajiinuaeye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akajionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." 2 Wathesalonike 2:3,4.

MASWALI YAKO YA KUTAFAKARI YAJIBIWA

1. Lakini Sabato sio ya Wayahudi peke yao?

   JIBU: La, Hasha, Yesu alisema, "Sabato ilifanyika kwa ajii ya mwanadamu." Marko 2:27. Siyo kwa Wayahudi tu, lakini kwa ajili ya wanaume na wanawake kila mahali. Wayahudi hawakuwepo hadi miaka 2500 baada ya Sabato kufanyika.

2. Je! 1Kor. 16:1,2 haizungumzii sadaka ya shule ya Jumapili?

   JIBU: La, Hasha, hakuna ushahidi wa mkutano wa hadhara hapa. Fehda ingetengwa faraghani nyumbani. Kulikuwa nanjaa katika Uyahudi (Warmi 15:26, Matendo 11:26-30) naye Paulo aliyaandikia makanisa ya Asia ndogo ili kuomba msaada. Hawa Wakristo wote waliitunza Sabato, hivyo Paulo akashauri kwamba Jumapili asubuhi, baada ya kupita sabato [wakati walipokuwa wakilipia madeni na kurekebisha akiba zao] waweke kando chochote kwa ajili ya ndugu zao wahitaji ili viwe tayari yeye atakapokuja. Lilipaswa kufanyika kwa faragha kama toleo la Kihispania linavyosema "nyumbani." Ufahamu pia, kwamba hakuna dokezo hapa la Jimapili kuwa siku takatifu. Kwa hakika, Biblia haishauri au kuamuru utunzaji wa Jumapili sehemu yoyote.

3. Je! Matendo 20:7-12 haithibitishi kwamba wanafunzi walitunza Jumapili kama siku takatifu?

   JIBU: Kulingana na Biblia kila siku inaanza wakati wa machweo nakumalizika siku inayofuata wakati wa machweo, (soma Mwanzo 1:5,8, n.k. na Walawi 23:32) na wakati wa giza wa siku ndio unaotangulia. Kwa hiyo ssabato inaanza Ijumaa jioni jua linapozama na kumalizika Jumamosi jioni jua linapozama. Mkutano huu wa Matendo 20 ulifanyika usiku wa Jumapili, au kile tunachoita leo usiku wa Jumamosi. [The New English Bible inaandika Matendo 20:7 hivi "Usiku wa Jumamosi katika mkutano wetu," n.k.]. Ulikuwa mkutano wa Jumamosi usiku, na uliendelea hadi usiku wa manane. Paulo alikuwa katika safari ya kuagana nao na alijua kwamba hatawaona tena watu hao kabla ya kifo chake (Fungu la 25). Hivyo si ajabu kwamba alihubiri kwa kirefu hivyo. [Hakuna huduma ya kawaida ya wiki ambayo ingeendelea hadi usiku.] Mkutano huu ulifanyika katika wakati wa usiku wa siku ya Jumapili – siku ya kwanza ya juma [au kile tunachoita leo Jumamosi usiku] kwa sababu Paulo "aliazimu kusafiri siku iliyofuata." Kule "kumega mkate" hakuna maana ya "siku takatifu," wala kwamba hawa Wakristo wa awali waliichukulia hivyo. Wala hakuna ushahidi wa mbali kwamba Sabato ilibadilishwa. Biblia huitaja Jumapili kama siku takatifu kwa sababu yoyote ile. Kwa nasibu, mkutano huu umetajwa katika maandiko kwa sababu tu ya muujiza wa kumfufua kijana aliyekuwa amepata ajali ya mauti wakati wa ibada hiyo.

4. Lakini je! muda haujapatozwa na siku za wiki kubadilishwa tangu siku za Kristo?
   JIBU: Hapana! Vitabu vikubwa vya maarifa na vitabu vya rejea vinavyoaminika vinaeleza wazi kwamba siku ya saba tuliyo nayo leo ndio ile ile Yesu aliyoitunza kuwa takatifu. Ni swala dogo tu la kuhakiki.

5. Je, Yohana 20:19 sio kumbukumbu ya wanafunzi kuanzisha utunzaji wa Jumapili kwa heshima ya Ufufuo?

   JIBU: Kinyume chake, wanafunzi hawa hawakuamini kwamba ufufuo ulikuwa umefanyika (Marko 16:14). Walikutanika pale kwa "hofu ya Wayahudi" na milango ilikuwa imekomelewa. Hakuna ishara yoyote kwamba waliihesabu Jumapili kuwa ni takatifu. Yapo mafungu kwamba waliihesabu Jumapili kuwa ni takatifu. Yapo mafungu manane tu katika agano jipya yanayotaja siku ya kwanza ya wiki. ["Jumapili"haimo katika Biblia]. Matano ya kwanza yanahusu Ufufuo: Math. 28:1, Mark. 16:2, matatu (Yoh. 20:19; Matendo 20:7, 1Kor. 16:12) katika awali lililotangulia. Hakuna hata moja linalosema kwamba Jumapili ni takatifu.

6. Je: Wakolosai 2:14-17 haiondolei mbali Sabato ya siku ya Saba?

   JIBU: Sivyo kabisa. Inazungumzia tu zile sabato zilizokuwa "kivuli cha mambo yajayo" na sio Sabato ya siku ya saba. Kulikuwa na siku takatifu au sikukuu kila baada ya miaka saba katika Israeli ya zamani ambazo pia ziliitwa Sabato. Hizi zilikuwa nyongeza, au "zaidi ya hizo sasbato za Bwana"(Lawi 23:38) au sabato ya siku ya saba. Hizi zote zilielekeza msalabani na zilikoma msalabani, lakini sabato ya Mungu ya siku ya saba ilifanyika kabla ya dhambi kuingia, na hivyo isingeweza kuwa kivuli cha jambo linaloluhusu ukombozi kutoka dhambini. Ndio sababu Wakolosai 2 hutofautisha na kutaja sabato zilizokuwa "kivuli." Hizi sabato za kila miaka saba ambazo zilikomeshwa zimeorodheshwa katika kitabu cha Mambo ya Walawi 23:4-44.

7. Kulingana na Warumi 14:5, siku tunayoadhimisha ni swala la mapendekezo ya mtu binafsi, ama sivyo?

   JIBU: Maneno “Kila siku” huelekeza katika siku sita za kazi. (Soma kutoka 16:4, 5, 26, n.k.) Sabato ya siku ya saba haihusiki. Majadiliano hapa ni kuhusu siku saba takatifu za mwaka, na maana yake baada ya msalaba. Fahamu kuwa sura yote inazungumzia kuhukumu (Soma fungu la 4, 13) kilamtu mwenzake. Paulo hasemi kama ni sawa au si sawa. Anasema “tusihukumiane.” (Warumi 7:7, 12,14; 1 Kor. 7:19; 9:21).

SIKU YA FURAHA

“Naliyangojea maneno yako kwa tumaini”

ZABURI 119:147

Mibaraka mikubwa imefungamanishwa na utunzaji wa Sabato, na Mungu anataka kwamba Sabato iwe ni siku ya furaha kwetu. Ilikuwa furaha Sabato ilipoanzishwa. Mungu alitazama kwa kuridhika, kazi ya mikono yake. Vitu vyote alivyokuwa ameviumba alitamka kuwa kila kitu ni “chema sana.” Mwanzo 1:31, Mbingu na nchi zilijawa na furaha. “Nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha.” Ayubu 38:7. Ingawa dhambi imeingia ulimwenguni kuharibu kazi yake kamilifu, Mungu bado anatupatia Sabato kama ushahidi kwamba Yeye, Mwenye uwezo wote, mwingi wa wema na rehema, aliviumba vitu vyote. Baba yetu wa mbinguni anahitaji kwamba kupitia utunzaji wa sabato ahifadhi miongoni mwa watu elimu kumhusu Yeye. Anakusudia kwamba Sabato ielekeze mawazo yetu kwake kama Mungu wa kweli aliye hai, na kwamba kwa kumjua Yeye tuwe na uzima na amani.

Bwana anasema “kama ukigeuza mguu wako usiihalifu Sabato, usifnye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya BWANA yenye heshima … ndipo utakapojifurahisha katika BWANA.” Isaa 58:13,14. Kwa wote wanaoipokea sabato kama ishara ya uwezo wa Kristo wa Uumbaji na ukombozi, itakuwa ni ya kupendeza. Wakimwona Kristo ndani ya Sabato wanajifurahisha katika yeye.

Mungu aliibariki na kuitakasa siku ya saba kwa sababu alistarehe katika siku hiyo kutoka kazi yake ya ajabu ya uumbaji. Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, na Mungu anamtaka aweke [kando] kazi zake katika siku hiyo, kama Yeye Mwenyewe alivyostarehe baada ya kazi ya siku sita ya uumbaji.

Mwanzoni tu mwa amri ya nne, Mungu alisema “Ikumbuke.” Anadai siku moja, aliyoitenga na kuitakasa. Anampatia mwanadamu kuw siku atakayopumzika kufanya kazi zake na kujitoa kuabudu na kukuza hali yake kiroho.

Sabato ni ishara ya uwezo wa uumbaji na ukombozi; hutueleza kwa Mungu kama asili pekee ya uzima na maarifa; hukumbusha utukufu wa mwanadamu wa asili, na hivyo kushuhudia kusudi la Mungu kutuumba upya katika mfano wake.

Sabato na familia vilianzishwa vyote katika Edeni, na katika kusudi la Mungu vimefungamanishwa pamoja milele. Katika siku hiyo, zaidi ya siku nyingine, inawezekana kwetu kuishi maisha ya Edeni.

Juu ya Sabato ameweka mkono wake wa rehema. Katika siku yake mwenyewe anatunza kwa ajili ya familia nafasi ya kushirikiana naye, na viumbe vya asili, na kilamtu na mwenzake.

Kwa kuwa Sabato ni ukumbusho wa uwezo wa uumbaji, hivyo ni siku zaidi ya siku nyingine zote tunayoweza kumjua sana Mungu kupitia katika kazi zake. Heri famili inayoweza kwenda mahali pa ibada siku ya Sabato kama Yesu na wanafunzi wake walivyokwenda katika Sinagogi – kwa kupita mashambani, kando kando ya ziwa au katika mahali penye miti mingi. Heri baba na mama wanaoweza kuwafundisha watoto wao neno la Mungu katika Maandiko na kwa vielelezo kutoka kurasa wazi za kitabu cha viumbe vya asili; wanaoweza kukusanyika chini ya miti ya kijani, katika hewa nzuri na safi ii kujifunza neno na kuimba sifa za Baba aliye juu.

Kwa maungano ya jinsi hiyo wazazi wanaweza kufunga watoto katika mioyo yao, na hivyo kwa Mungu vifungo visivyoweza kuvunjika.

Sabato ni kifungo cha dhahabu kinachomuunganisha Mungu na watu wake. Kwetu kama ilivyokuwa kwa Israeli Sabato imetolewa kama “agano la milele.” Kwa wale wanaoiheshimu siku yake takatifu, Sabato ni ishara kwamba Mungu anawatambua kama watu wake wateule. Ni ahadi kwamba atatimiza agano lake kwao. Kila roho inayopokea ishara ya serikali ya Mungu hujiweka chini ya agano takatifu la milele. Anajifunga katika mnyororo wa dhahabu wa utii, ambao ni kila pete ni ahadi. Historia iliyopita ya kusudi la Mungu, inahitajika kuweka mbele ya watu wake mara kwa mara, wazee kwa vijana. Kila mara tunahitaji kuelezea tena na tena wema wa Mungu na kumsifu kwa kazi au matendo yake ya ajabu.

Sabato na familia vilianzishwa vyote
Katika Edni, na katika kusudi la Mungu
Vimefungamanishwa pamoja milele. Katika
siku hiyo, zaidi ya siku nyingine
yoyoe, inawezekana kwetu
kuishi maisha ya Edeni.

Kanisa la Mungu hapa duniani ni moja na kanisa la Mungu lililo juu. Waumini hapa duniani na viumbe vilivyo mbinguni ambavyo kamwe havikuanguka dhambini hufanya kanisa moja. Kila kiumbe chenye akili ya juu cha mbinguni kina moyo wa kupenda kushirikiana na kusanyiko la watakatifu duniani wanaokusanyika kumwabudu Mungu.

Kadri mnavyokusanyika Sabato hata Sabato, imbeni sifa kwake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.

Hekalu la Mungu limefunguliwa mbinguni, na mlango umefurika utukufu ambao ni kwa ajili ya kila kanisa litakalompenda Mungu na kuzishika amri zake. Tunahitaji kujifunza, kutafakari, na kuomba. Ndipo tutakuwa na macho ya kiroho ilikutambua vyumba vya ndani vya hekalu la mbinguni. Tutapata kufahamu somo kuu la wimbo na shukrani za kwaya ya mbinguni inayokizunguka kiti cha enzi. Tunapotumia dawa ya macho ya dhahabu tutauona utukufu ule ujao. Imani itapenya katika vivuli vizito vya shetani, na tutamwona mtetezi wetu akijifukiza uvumba wa haki yake Mwenyewe kwa ajili yetu. Tutakapoona jambo hili kama

lilivyo hasa, kama Bwana anvyokusudia tulione, tutajazwa na ufahamu wa ukuu usio kifani na wingi wa upendo wa Mungu.
Mungu anatufundisha kwamba imetupasa kukusanyika katika nyumba Yake ili kukuza tabia za upendo mkamilifu. Hili litawafanya wakaaji wa dunia wastahili kwa ajili ya makao ambayo Kristo amekwenda kuwaandalia wote wampendao. Kule watakusanyika hekaluni Sabato hata Sabato, na mwezi mpya hata mwezi mpya, kuungana katika muziki bora sana wa nyimbo za kumsifu na kumshukuru Yeye aketiye juu ya kiti cha Enzi, na yeye Mwana-Kondoo milele na milele.

Karibu, siku ya utukufu ya Sabato

Salaam, siku ya amani! Iliyobarikiwa na Mungu!
Kwa kupendezwa tutauimba utukufu wako,
Kumbukumbu ya lile pumziko takatifu
La Mfalme mkuu wa viumbe vyote:
Wakati huu mtakatifu mwandamu amepewa,
Utabiri wa furaha kamili ya mbinguni.

Sikiliza! Hadi kufikia baraza za juu zing'aazo
Sifa za shangwe jinsi gani zinasikika sasa!
Kuzunguka ile sheria takatifu ya upendo
Maserafi kwa heshima wanasujudu;
Hebu dunia, kwa kuitikia muziki huo,
Ilitukuze jina takatifu la Mungu pekee.

Ukaribie, ewe siku ing'aayo, isiyokuwa na mwisho!
Wakai wote wanapomtukuza katika hekalu lake,
Na kushikilia uongozi wake wa ulimwengu
Tangu kizazi hadi kizazi, milele zote;
Ndipo Sayuni itatawala kwa ushindi,
Na Edeni itachanua tena duniani.

Na kijana mtunza Sabato
Annie R. Smith
1828-1855

MPANGO WA MUNGU WA AJABU

Baada ya mwandamu kutenda dhambi, ahadi ya mwokozi ilitolewa na sadaka za kutekelezwa zilielekeza kwa kifo cha Kristo. Mungu aliinua kundi maalum la watu aliowafanya kuwa taifa la Israeli. Aliwatunza, aliwapenda, na kuwaongoza watu wake kwani aliwakusudia jambo kubwa. Agizo la tohara likawa ishara ya ahadi yao kuwa wakweli, na wafuasi watiifu wa Mungu. Maisha yao yalipaswa kuongozwa na kanuni za neema ili kuonyesha ulimwengu faida ya imani inayotii. Hivyo Mungu akafanya agano nao – mapatano au mkataba.

AGANO LA KALE

Sehemu ya Mungu:

- Aliahidi kubariki watu wake
- Atawapa urithi wa nchi ya Kaanani
- Atawafundisha mapenzi yake
- Atawatumia Masihi
- Atawatumia wao kumtangaza Kristo.

(Kumb. 11:22-27; 4:13; Mwanzo 12:1-3; Kutoka 19:5,6)

Sehemu ya Israeli:

Watu walitakiwa kutii na kushirikiana na matakwa yote ya Mungu. Hili lingefanyika kwa kupokea neema na uwezo wa Mungu maishani mwao. (Kut. 19:4-6; Kumb. 4:13,36-40).

Lilifanyika lini? Lilifanyika kwanza na Ibrahimu na katika uzao wake likawa na maana kamili kabisa. (Mwanzo 12:1-3).

Lilitiwaje muhuri? Kwa damu ya kafara. (Kutoka 24:5-8).

Lilivunjaje? Kwa kumkataa na kumsulubisha Kristo Wayahudi walivunja agano na wao wakakataliwa kama taifa teule. (Math. 21:43)

Kama Israeli wangekuwa waaminifu kwa Agano la Kale nini kingetokea? Agano la kale lilikusudiwa kuwawezesha wale waliokuwa chini yake kufanywa tayari kuingia katika haki na wajibu wa agano jipya au la Milele. Wangeweza kupewa furaha ya wokovu katika Yesu. Lakini jambo la huzuni ni kwamba bado wanamsubiri Masihi na hawakuona na kuipokea kafara ya upatanisho ya Mwana wa pekee wa Mungu.

Sehemu ya Mungu:

- Aliahidi kubariki watu wake
- Ataandika sheria yake katika nia na mioyo yao
- Atakuwa Mungu wao
- Tutakuwa watu wake. (Waebrania 8:8-10)

Sehemu yetu:

Kuwa watiifu kwa maagizo yote ya Mungu. Hili litafanyika kupitia Kristo na uhusiano wetu wa karibu sasna naye – si kwa nguvu zetu wenyewe, bali kwa kumtegemea Kristo na nguvu zake. (Warumi 9:31-33; Wafilipino 4:13; 3:9; Ufunuo 12:14). Lilifanyika lini? Kristo aliposulubiwa Mungu alihamishia haki na wajibu wa uhusiano wa agano kwa watu wake, wateule wapya, yaani kanisa la Kristo. (Wagalatia 3:27-29). Lilitiwaje Muhuri? Kwa damu ya Yesu alipokufa msalabani. (Luka 22:20; Waebrania 9:14,15).

Tofauti ni ipi? Tofauti kuu ni kwamba “Agano la Kale” lilifanywa pamoja na Waisraeli kama taifa, lakini “Agano Jipya” linafanyika na watu binafsi wanaomwamini Kristo.

Published by:

Leaves of Life – International
P.O. Box 17
Mafinga Iringa Tanzania East Africa